# DHIMA ZA NYIMBO KATIKA MATAMBIKO YA JAMII YA WATU WA MKOA WA KUSINI UNGUJA

**HIDAYA JUMA MUSSA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KAMA SEHEMU YA KUTIMIZA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) YA KISWAHILI KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2023**

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo: **“Dhima za Nyimbo katika Matambiko ya Jamii ya Watu wa Mkoa wa Kusini Unguja”** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya Umahiri ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…………………………………………………

**DKT. FELISTAS R. MAHONGE**

**(Msimamizi)**

Tarehe : …........................................................

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya Tasnifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha mwandishi Mkuu au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## TAMKO

Mimi **Hidaya Juma Mussa** nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyengine.

Saini ________________________

Tarehe ________________________

## TAMKO

Mimi, **Hidaya Juma Mussa,** nathibitisha kwamba, tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Digrii yoyote.

______________________________

**Hidaya Juma Mussa**

______________________________

Tarehe

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapenzi, Bibi Mwanamrisho Rajabu na Bwana Juma Mussa, waliojitolea kwa hali na mali hadi kufikia umri huu. Kwa mapenzi yao kwangu na kunisomesha hadi leo nimefikia hatua hii kitaaluma. Kwa pamoja nawatunukia zawadi hii ipokeeni. Asanteni.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kutoa shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu Allah Subhanahu Wataalah kwa kunijaalia afya njema kipindi chote cha masomo yangu, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili, Alhamdulillah. Pili, shukurani za pekee ni kwa wazazi wangu. Bi. Mwanamrisho Rajabu na Bw. Juma Mussa, kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha na kwa uvumilivu wao kuwa mbali nami hasa katika kipindi chote nilichokuwa nikijishughulisha na masomo yangu ya uzamili. Nawaombea maisha marefu yenye afya na baraka tele. Tatu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Msimamizi wangu Dkt. Felistas Mahonge kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Kunifunza na kunipa miongozo juu ya mada yangu ya dhima ya nyimbo za matambiko Namuombea afya njema na maisha marefu ili awe hazina kwa ya wenye kiu ya kutafuta taaluma. Nne, napenda wote walioshiriki katika utafiti huu kwa ukarimu na ushirikiano walionipa kipindi chote cha utafiti wangu. Namshukuru Dkt. Mohammed Omary Maguo kwa kunifunza lugha ya Kiswahili na kunipa changamoto za kitaaluma juu ya utafiti huu unaohusu matambiko kwa mswada wake wa fasihi ya Kiswahili ambao ulinipa chachu ya kutafuta data katika utafiti huu. Pia nitakuwa mchache wa fadhila nisipotoa shukurani kwa wanaidara wote wa idara ya lugha na fasihi kwa maoni na miongozo yao hadi leo nimefanikiwa. Mwisho napenda kumshukuru mume wangu mpendwa kwa ustahamilivu wake kwa kipindi chote cha mahangaiko ya masomo hasa baadhi ya siku nikiwa sipokuwa nawe.

## IKISIRI

Utafiti huu umechunguza dhima zaa nyimbo za matambiko katika jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja. Lengo hilo lifikiwa kwa kubainisha nyimbo za matambiko zilizopo katika jamii ya watu wa Makunduchi. Sambamba na kubainisha mahali, wakati na jinsi nyimbo zinavyotumika katika Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha, uchunguzi wa dhima zinazojitokeza katika nyimbo za matambiko katika jamii ya watu wa Mkoa wa Kusini zilifafanuliwa. Utafiti huu ulifanyika uwandani kwa kushuhudia, kuhoji na kudodosa ili kukusanya data kutoka vyanzo tofauti vya watafitiwa. Utafiti huu ulifanyika katika Kisiwa cha Unguja, Mkoa wa Kusini, Wilaya Kusini katika kijiji cha Makunduchi, Uchambuzi wa data za wa utafiti huu ni wa mkabala wa kimaelezo hii ni kutokana na aina ya utafiti pamoja na sampuli iliyotumika. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni ya Simiotiki na ya Uhalisi mazingaombwe. Nadharia mbili hizi zimetumika ili kusaidia katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa tambiko ni amali muhimu katika ustawi wa maisha ya watu wa Kusini Unguja kwa sababu tambiko limetumika katika shughuli nyingi muhimu za kijamii. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa nyimbo za tambiko zipo za aina tofauti kama vile, za kukaribisha mizimu, maamkizi, dua, na kuomba shifa. Pia, eneo la utendekaji ni pwani, kwenye miti mikubwa, mapango na kwenye uwanja.

**Maneno Muhimu:** *Mizimu*, *Tambiko, Nyimbo*

# YALIYOMO

ITHIBATI ........ ii

HAKIMILIKI ........ ii

TAMKO ........ iii

TAMKO ........ iv

TABARUKU ........ v

SHUKRANI ........ vi

IKISIRI ........ vii

YALIYOMO ........ viii

VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........ xiii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ........ 1**

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........ 8

1.4 Malengo ya Utafiti ........ 9

1.4.1 Lengo Kuu ........ 9

1.4.2 Malengo Mahsusi ........ 9

1.5 Masuali ya Utafiti ........ 9

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 9

1.7 Mipaka ya Utafiti ........ 10

1.8 Mpangilio wa Tasnifu ........ 10

**SURA YA PILI : MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........ 12**

2.1 Utangulizi ........ 12

2.2 Maandiko Kuhusu Nyimbo ........................................................................ 12
2.3 Tafiti Zilizofanywa Kuhusiana na Nyimbo ............................................... 15
2.4 Maandiko Kuhusu Matambiko .................................................................. 17
2.5 Tafiti Zilizofanywa Kuhusiana na Matambiko .......................................... 19
2.6 Nadharia ya Semiotiki................................................................................ 22
2.6.1 Mapungufu Yaliyobainika Katika Nadharia ya Simiontiki ........................ 26
2.6.2 Nadharia ya Uhalisiamazingaumbwe........................................................ 26
2.7 Mkabala wa Nadharia ya Utafiti ................................................................ 29
2.8 Pengo la Maarifa ........................................................................................ 29
2.9 Hitimisho.................................................................................................... 30

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI NA VIFAA VYA UTAFITI............. 31**

3.1 Utangulizi................................................................................................... 31
3.2 Eneo la Utafiti ............................................................................................ 31
3.3 Mbinu za Utafiti ......................................................................................... 31
3.4 Kundi Lengwa............................................................................................. 32
3.5 Sampuli na Usampulishaji .......................................................................... 32
3.6 Ukusanyaji wa Data ................................................................................... 32
3.6.1 Data za Awali.............................................................................................. 32
3.6.2 Data za Upili ............................................................................................... 33
3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ................................................................... 33
3.7.1 Mbinu ya Ushuhudiaji................................................................................. 33
3.7.2 Mbinu za Usaili ........................................................................................... 34
3.8 Uchambuzi wa Data ................................................................................... 34

3.9 Usahihi wa Utafiti ..... 35

3.10 Maadili ya Utafiti ..... 35

3.11 Zana na Vifaa vya Utafiti ..... 36

3.11.1 Kompyuta ..... 36

3.11.2 Kalamu na Karatasi ..... 36

3.12 Muhtasari ..... 37

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ..... 38**

4.1 Utangulizi ..... 38

4.2 Nyimbo za Matambiko Zilizopo katika Jamii ya Watu wa Makunduchi. ..... 38

4.2.1 Wimbo wa Kuingia Matambikoni ..... 38

4.2.2 Kuwakaribisha Wageni ..... 40

4.2.3 Wimbo wa Kuomba Mvua ..... 42

4.2.4 Wimbo wa Kuombewa Ulinzi na Amani Kwa Wanandoa ..... 44

4.2.5 Mwimbo wa Kuomba Kupata Mtoto ..... 45

4.2.6 Wimbo wa Kuomba Neema na Baraka ..... 46

4.2.7 Mwimbo wa Kufukuza Ugonjwa na Kuomba Afya Njema ..... 47

4.2.8 Wimbo wa Ufunguzi wa Pungwa ..... 48

4.2.9 Wimbo wa Kumtambika Mtoto ..... 49

4.3 Mahali, Wakati na Jinsi Nyimbo Zinavyotumika katika Mkoa wa Kusini Unguja ..... 49

4.4 Matambiko Yanayofanyika Pwani ..... 50

4.4.1 Matambiko Yanayofanywa Kwenye Miti Mikubwa ..... 51

4.4.2 Tambiko Linalofanyika kwa Kuzunguka Mji ............................................. 52

4.4.3 Matambiko Yanayofanyika katika Makaburi ............................................. 53

4.4.4 Matambiko yanayofanyika Mapangoni ..................................................... 54

4.5 Dhima Zinazojitokeza katika nyimbo za matambiko ya Jamii ya Watu wa Mkoa wa Kusini Unguja ........................................................................... 55

4.5.1 Matambiko Huwafanya Wanajamii Kuwa na Utii....................................... 55

4.5.2 Kujenga Heshima za Koo ........................................................................ 56

4.5.3 Ushirikiano Katika Kazi............................................................................. 57

4.5.4 Nyimbo Hutumika kwa Lengo la Tiba ....................................................... 58

4.5.5 Kuendeleza Utamaduni wa Jamii.............................................................. 59

4.5.6 Kujenga Tabia ya Uvumilivu ..................................................................... 60

4.5.7 Dhima za Mapenzi na Ndoa....................................................................... 61

4.5.8 Kutoa Wasia kwa Wanadoa ....................................................................... 64

4.5.9 Dhima ya Usafi ......................................................................................... 65

4.5.10 Kuondoa Shida ....................................................................................... 66

4.6 Hitimisho.................................................................................................... 68

**SURA YA TANO: MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO .......... 69**

5.1 Utangulizi.................................................................................................... 69

5.2 Muhtasari wa Utafiti .................................................................................. 69

5.3 Matokeo ya Utafiti kwa kila lengo............................................................... 70

5.3.1 Lengo la Kwanza ..................................................................................... 70

5.3.2 Lengo la Pili.............................................................................................. 70

5.3.3 Lengo la Tatu ........................................................................................... 71

5.4 Matokeo ya Jumla ........ 71

5.5 Mchango wa Utafiti ........ 72

5.6 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ........ 73

5.7 Hitimisho ........ 73

**MAREJELEO…… ........ 74**

**VIAMBATANISHO ........ 80**

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| BAKITA | Baraza la Kiswahili Tanzania |
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| HT | Haina Tarehe |
| KHJ | Keshatajwa Hapo Juu |
| Mw | Mwalimu |
| SA | Swalallahu Alaihi Wassalama (yaani Rehema na Amani za Mwenyezi- Mungu Zimshukiye juu yake Mtume) |
| SW | Subuhanahu Wataala (Mwenyezi-Mungu Aliyetukuka kwa utukufu wake) |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UK | Ukurasa |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura ya kwanza imefafanua vipengele vya usuli wa mada, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, na mpangilio wa utafiti

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Nyimbo ni dhana kongwe zaidi inayotumia utungo ulio na mdundo, mahadhi na unaoweza kuimbika. Hali hiyo inazifanya nyimbo ziwe na umaarufu mkubwa katika jamii nyingi za Kiafrika na shughuli chache wazifanyazo wanadamu ndio haziambatani na nyimbo (Ngure, 2003:72). Pia, BAKITA (2015: 1176) wanasisitiza kuwa nyimbo ni "tungo fupi za kimuziki zenye maneno yaliyopangwa ambayo hunenwa kwa mpangilio pamoja na ala au vyombo mbalimbali vya kuchezea. Aidha, Mulokozo, (1996) anashadidia kuwa nyimbo ni tungo za kisanaa zinazowasilishwa kimuziki kwa kutumia sauti iliyo katika mpangilio fulani wa mahadhi, melodi na zenye mapigo ya kiurari. Hali inayozingatiwa kuwa nyimbo ni hitaji maalumu la kimaisha la mwanadamu.

Historia inaonesha kuwa nyimbo[1] zilikuwepo tangu alipoumbwa mwanadamu kupitia mfumo wa ushairi. Nyimbo hizo zilianza kutokana na hisia za matukio

[1] Zilishika kasi wakati ambapo mwanadamu alipoanza kuzitumia katika harakati za kujitafutia mahitaji ya maisha ya kila siku. Nyimbo hujitokeza katika miegamo ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii kwa mujibu wa matakwa ya mtu. Mgawanyo wa nyimbo upo wa aina nyingi miongoni mwa hizo ni nyimbo za kazi, tohara, kujiburudisha, harusi, uzawa wa mtoto na nyimbo za mapenzi, za marika ya Wazee na vijana. Kila jamii huzipa nyimbo hizo majina tofautitofauti kwa mujibu wa matakwa na miegamo ya matukio ya kila sikukatika jamii hizo (Ngure, 2003; Mulokozi, 1975; Mulokozi 2017; Omar, 2008).

yaliyowakumba wanadamu katika mazingira yao, ugumu wa kujituma na ushujaa. Katika jamii nyingi za ulimwenguni nyimbo zilianza wakati mwanadamu alipobuni lugha iliyomtoa katika hali ya uhayawani na kumfanya awe kiumbe razini anayetofautisha mambo mbalimbali yanayotokea maishani mwake (Senkoro, 1987; Njogu, na Chimerah, (1999); Ngure, 2003; Mulokozo, (2017). Mawazo ya wataalamu hawa yanathibitisha kuwepo kwa historia ndefu ya nyimbo duniani.

Nyimbo za matambiko zimeanza kuimbwa tangu mwanadamu alipoanza kufanya matambiko ya aina mbalimbali duniani. Historia inaonesha kuwa utamaduni wa kuimba nyimbo za matambiko umefungamanishwa na ushirikina, matendo ya ajabuajabu na mandhari tatanishi anayokaa mwimbaji husika. Hali hiyo inazifanya nyimbo za matambiko kuwa maarufu katika jamii nyingi za Kitanzania. Mdhihiriko na mitindo ya uimbaji wa aina mbalimbali wa nyimbo za matambiko huambatana na mambo ya jadi ya asili ya jamii husika hususani katika jamii ya mkoa wa Kusini Unguja. Kwani kila mkoa hutofautiana kwa namna moja au nyingine ya uimbaji wa nyimbo za matambiko. Nyimbo hizo hubeba dhima za aina mbalimbali kutegemeana na maudhui inayoambatana nayo. Nyimbo za matambiko zimebeba thamani kubwa kwa maendeleo ya utamaduni wa jamii ya Zanzibar na mkoa wa Kusini Unguja. Nyimbo hizo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za Kiafrika kwa vile hutumika kwa dhima za aina mbalimbali kisiasa, kiuchumi na kitamaduni. Hali hii hutegemea maudhui chomozi ya uimbaji wa nyimbo husika (Ngure, 2003).

Matatizo kadhaa yanayohatarisha nyimbo za matambiko kuimbwa kupitia kipengele cha fasihi simulizi yamejitokeza katika nyanja mbalimbali. Mosi, uwasilishaji wa

asili wa kuimba kwa mdomo katika matambiko umepungua sana kwa dhana kuwa nyimbo za matambiko zimepitwa na wakati. Pili, uhifadhi wa kichwani umepungua kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Ukuaji ulioleta mabadiliko ya kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia umezidisha hatari ya kudumaa kuimbwa kwa nyimbo za aina mbalimbali za matambiko. Tatu, shehrehe za matambiko zimeanza kupotea kutokana na watu wengi kutoamini ibada hizi. Hasa pale masheikh walipoanza kukemea na kuihusisha tambiko kama ushirikiana ambao Allah (SW) amekataza.

Matambiko ni dhana pana inayoegemezwa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Hali inayothibitisha kuwa matambiko hutendwa kila siku ndani ya maisha ya mwanadamu. Upo ugumu wa kuyatenganisha maisha ya asili ya Mbantu na suala la ibada za wahenga" zinazohusiana na matambiko ya aina mbalimbali (Chuachua, 2016: 13). Pia, TUKI (2001:10) inathibitisha kuwa matambiko hufanywa kulingana na muda na utaratibu maalumu katika jamii husika. Hivyo, matambiko ni shughuli za kimila zinazofanywa katika kipindi au muda fulani unaowekwa na jamii ya watambikaji

Historia inabainisha kuwa matambiko[2] yameanza zamani tangu karne ya 3 BC, katika nchi za Ulaya, Ufaransa na India. Katika karne hiyo inakisiwa kuwa

[2] Jamii nyingi za Waafrika hufanya matukio na matendo mbalimbali yanayothibitisha kuwapo kwa kitu au jambo fulani katika jamii husika; ikiwemo ontolojia za aina mbalimbali na matumizi yake. Kwa kawaida, kila jamii huwa na ontolojia zinazodhihirisha kuwapo kwa mila, matambiko, desturi, na silka za watu wa jamii husika kutokana na mienendo, tamaduni zao na matumizi ya ontolojia ya falsafa ya Kiafrika kwa mujibu wa jamii husika. Kwa mujibu wa Chuachua (2016:8) anaeleza kuwa Ontolojia ni taaluma ya falsafa inayoshughulikia asili ya kuwapo au kuishi, kategoria za kuwapo pamoja na mahusiano yake. Hivyo, ontolojia hujishughulisha kujibu maswali, kama vile; vitu vilivyokuwapo ni vipi au vinavyosemekana kuwapo ni vipi? Vilivyokuwapo vinawezaje kuwekwa katika makundi huku vikihusianishwa kulingana na viwango vya kidarajia pamoja na kufanana au kutofautiana kwao?

alikuwepo nabii Idrisa[3]. Wafuasi wa nabii Nuhu waliyaendeleza matambiko na kuyaendeleza duniani kote (Ali 2014). Pia katika nchi za China, Ugiriki na Rom usihiri ulishika kasi katika karne ya kumi na nne na kumi na tano (Abdahu, 2011:35-65)[4]. Hapa watu walianza kufuga majini, kumiliki mizimu na majini na mashetani walitazamwa kama viumbe wenye karama za aina mbalimbali hadi kufanyiwa matambiko kwa mujibu wa matakwa ya watambikaji (Billig 2005:12)

Wayunani walifanya matambiko na kuhadithiana yale yaliyojiri katika jamii yao, kuandikwa vitabuni; vikiwemo riwaya ushari, tamthiliya na hadithi fupi. Baadaye wasanii waliigiza na kuonesha matambiko ya aina mbalimbali kupitia fikra zao kwa mujibu wa matukio yaliyomo katika jamii hiyo.

Ilipofika karne ya kumi matambiko kupitia wafuasi wa Nabii Nuhu. Hii ni kutokana na shetani kuwazaini watu na kuwashawishi watengeneze masanamu ya watu watukufu na wayaweke katika njia mbalimbali kasha wayaabudia masanamu hayo na kuyafanyia matambiko ya aina mbalimbali uendeleza Al-Maqqarī (1840) Pia matambiko hayo yalifanikishwa kuombwa miungu ya Babeli waliowakilishwa kwa alama na namba 7 au joka lenye vichwa 7 kwani ndilo lililotawala miungu wote 36 wa matambiko walioitwa Decans. Na Mungu aliyekuwa mtawala mkuu wa matambiko yote wote alikuwa Mungu Jua (Gideon, 2020: 21).

---

[3] Ni babu wa baba wa nabii Nuhu. Ni mtume wa mwanzo kutazamia nyota pamoja na kuzijua hesabu zake. Utumiaji huo wa nyota ulikuwa ni mojawapo ya miujiza aliyopewa na Mwenyezi-Mungu. Pia, mtume huyo ni wa mwanzo kuandikia kalamu, ushonaji wa nguo, uvaaji na utengenezaji wa nguo kwani hapo kabla watu walikuwa wakivaa ngozi. Aidha, walitengeneza mizani, vipimo na silaha za mapambano ya vita. (Abdahu, 2011: 35).

[4] https://en.wikipedia.org/wiki/Muhammad_Abduh

Ilipofika mwishoni mwa karne ya 17 na 18 matambiko ya kisasa yalifanywa na mtu mmoja mmoja au jamii nzima. Katika karne ya 20 matambiko yalichukuliwa kama chombo cha kufikisha maombi ya wanadamu kwenda kwa mungu, kujikinga na mpotoko wa maadili na itikeli za jamii husika. Ilipofika karne ya 21 ya sayansi na teknolojia matumizi ya matambiko yamepungua ingawa bado yanaendeshwa katika jimii nyingi za Kiafrika kupitia nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii (Sengo, 1975)

Kwa upande wa Afrika matambiko yanakisiwa kuingia katika karne ya nne kupitia nchini Misri, Sudani, Iraq na maeneo yote Bara Arabu (Gideon, 2020; *Islamic Propagation Centre*, 2009). Sababu iliyochochea kuenea kwa matambiko hayo ilitokana na njaa na ukame katika jamii za Afrika, ambapo, matatizo hayo yaliwafanya watu kufanya matambiko na kuomba mizimu.

Vilevile, Masebo (2013) anaendelea kusema kuwa, katika jamii nyingi za Kiafrika matambiko bado yanachukuliwa kuwa na umuhimu mkubwa sana. Jamii nyingi hufanya matambiko pale vinapotokea vifo vya kutatanisha, magonjwa yasiyoeleweka, ukame, na hata ajali, kwa ajili ya kuomba msamaha kwa mababu waliotangulia. Katika baadhi ya makabila kama vile Mniha, Wahezabi, Wanyisanzi na Wanyiramba hutambika katika mapango, milima na sehemu zenye miti mikubwa kwa ajili ya kutatua shida zao kama maradhi, vifo na ukame.

Ibada hizi za miungu zinazoambatana na matambiko hazipo tu katika bara la Afrika, bali zipo katika mabara mengi na jamii nyingi duniani, hata katika jamii ya Ibrahimu baba wa imani kulikuwa na ibada za mizimu, yaani Ibrahimu pia baba wa imani,

rafiki wa Mungu alitoka katika jamii iliyokuwa inaabudu miungu. Biblia inavyosema katika (Yoshua 24:1-3) yafuatayo :-

> Yoshua akawakusanya kabila zote za Israili huko Shekemu Akawaita Wazee wa Israili na wakuu wao, na waamuzi, Na maakida wao nao wakahudhuria mbele za Mungu. Yoshua akawambia watu wote, Bwana Mungu wa Israili Asema hivi. Baba zenu hapo zamani walikaa ng'ambo ya mto. Baba yake Ibrahim na baba yake Nahori Wakaitumikia miungu mingine. Nami nikamtwaa Ibrahimu baba yenu toka kando ya mto, nikamuongoza katika nchi yote ya Kanaan. (Yoshua, khj)

Mara nyingi, matambiko hufanyika kuambatana na kafara. Baadhi ya makabila huweza kuchinja wanyama, wengine hutumia pombe na kadhalika. Kimsingi kafara linatolewa kwenye tambiko hutegemea na kabila. Nchi ya Tanzania yapo makabila mbalimbali yanayofanya jadi hii ya matambiko kwa lengo la kuondoa matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii. Makabila ya maeneo ya Tanga, Pwani na Morogoro hufanya matambiko yao makaburini, kwenye miti mikubwa, milimani, mapangoni, ziwani, baharini, makaburini na maporini. Katika shughuli hizo majina maalumu ya mababu hutolewa. Matambiko huhusisha nyimbo tofauti zinazoimbwa na wanajamii na nyimbo hizo huimbwa kutokana na dhumuni la tatizo

Kwa upande wa Zanzibar, matambiko[5] yalianza zamani sana tangu enzi za mabibi na mababu zetu kama ilivyo kwa jamii nyingine duniani. Matambiko hayo yalifanyika kupitia shughuli maalumu kama vile maombi, ukame, vifo na magonjwa yasiyoeleweka. Matambiko yametumika katika harakati za mwanadamu. Matambiko

[5] Yalianzishwa kupitia shughuli za maombi ya vifo, magonjwa yasiyoeleweka.na ufanyaji kwa kurithiwa kizazi hadi kizazi ili kuweza kuendeleza mila na utamaduni waliourithi (Kapinga. 2017).

ayo yalifanyika kutokana na mambo yalikuwa nje ya uwezo wa jamii husika. Kama vile ukame, vifo, mafuriko, radi na magonjwa. Kwa hiyo matambiko yalifanywa ili kuomba msaada kwa Mungu awapatie nafuu juu ya shida husika. Utaribu huu ulirithishwa kizazi hadi kizazi (Masebo, 2013)

Zipo jamii zinazofanya matambiko siku maalumu kila mwaka. Kwa mfano Kusini mwa Unguja katika kijiji cha Makunduchi[6] hufanya matambiko ya kila Mwaka katika siku maalumu. Miongoni mwa matambiko yanafanyika siku maalumu yam waka ni matambiko ya Mwaka kongwa. Tambiko hili kama ilivyo mengine huambatana na nyimbo. Hivyo mtafiti ameona ipo haja ya kuchunguza dhima za nyimbo katika matambiko ya watu wa mkoa Kusini Unguja ili kuangalia uhalisia uliopo baina ya dhima za nyimbo za matambiko na hali uhalisia uliopo baina ya dhima ya nyimbo za matambiko na matukio halisi ya kijamii (Asumta, 2011).

Jamii ya mkoa wa Kusini Unguja ni miongoni mwa jamii ya Zanzibari, yenye kuendeleza matambiko ya aina mbalimbali; hususani katika kijiji cha Makunduchi. Matambiko hayo hufanywa kupitia Mwaka Kongwa kwa kila mwaka. Matambiko hayo hufanyika katika sehemu mbalimbali katika mkoa huo. Miongoni mwa sehemu mashuhuri zinazofanyika matambiko hayo kama vile  mzimu wa maji pepo, Kijiwe Shomoo kilichopo Kusini Makunduchi, pia mzimu wa mapopwe, Msikiti kichaka, kwa Biti Khatibu ambayo ipo katikati ya mji wa Makunduchi. Kwa upande wa Kaskazini ni eneo la Kajengwa pia upo mizimu wa Mwampambe, Kipanga ngoma na Mabuko. Matambiko hayo hufanyika kutokana na imani ya wanajamii wa Mkoa wa

[6] Makunduchi ni mji ulio na vijiji na viambo vingi; mji huu upo wila ya kusini, Mkoa wa Kusini Unguja ambao umepakana na bahari ya hindi. Kwa upande wa mashariki bahari hiyo inaitwa Kigaeni na upande wa Kaskazini inaitwa Shungi na Kusini bahari hiyo inaitwa Pwani ya Kusini (Issa, 2018: i).

Kusini Unguja kuwa mizimu inayopatikana katika Mkoa huo inakuwa na nguvu za ziada katika kuendeleza maisha yao na kutatua matatizo yaliyowakabili (Khamis, 2008). Maelezo ya mtaalamu huyu yalimsadiwa mtafiti kuyafahamu baadhi ya matambiko yaliyoko Mkoa wa Kusini unguja

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Nyimbo za matambiko zimekuwa zikifanya kazi ya kusawiri maisha halisi ya jamii ya watu ya Visiwani na Waswahili kwa ujumla. Kutokana na kuisawiri jamii ilivyo, nyimbo hizo zimekuwa ni chombo imara katika kujenga maadili ya jamii. Watafiti wengi wamezungumzia katika tafiti zao suala la nyimbo katika mitazamo tofauti baadhi yao ni Zaharia (2007), Mohammed (2014), Gora (2011), Thabit (2007), Safya (2007), Salim (2009) watafiti hao kama wawakilishi wa wengine wamechunguza mitindo ya nyimbo za uganga wa pepo, maudhui ya nyimbo za taarabu katika jamii ya watu wa Zanzibar, athari za nyimbo za arusi kwa mke na mume. Pia katika tafiti hizo wamegundua mambo mbalimbali kama vile nyimbo za taarabu zinasaidia katika kudumisha mila na maadili ya jamii hususan jamii ya Zanzibar. Vilevile, wamegundua kupitia nyimbo jamii inaweza kubadili tabia zao katika mienendo mibaya kuja katika tabia nzuri. Ijapokuwa watafiti hawa wamefanya tafiti hizo na kutoa mchango mkubwa mtafiti amegundua hakuna utafiti uliofanya kuhusu kuchunguza dhima ya nyimbo katika matambiko ya jamii ya watu wa mkoa Kusini Unguja katika jamii ya Makunduchi jambo ambalo limempa msukumo mtafiti wa utafiti huu kufanya utafiti huo ili kuangalia dhima ya nyimbo za matambiko katika jamii ya Wamakunduchi na jinsi zinavyoendana na maisha halisi jamii.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo makuu mawili lengo kuu na malengo mahsusi

### 1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza dhima ya nyimbo za matambiko katika jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

i. Kubainisha nyimbo za matambiko zilizopo katika jamii ya watu wa Kusini Unguja.
ii. Kubainisha mahali, wakati na jinsi nyimbo za matambiko zinavyotumika katika mkoa wa Kusini Unguja
iii. Kuchambua dhima zinazojitokeza katika nyimbo za matambiko ya jamii ya watu wa mkoa wa Kusini Unguja

## 1.5 Masuali ya Utafiti

i. Ni nyimbo zipi zinazoimbwa katika matambiko ya jamii ya watu wa mkoa Kusini Unguja.
ii. Ni wapi, wakati gani nyimbo za matambiko ya jamii ya watu Mkoa wa Kusini Unguja huimbwa.
iii. Dhima zipi zilizopo katika nyimbo za matambiko ya watu wa mkoa Kusini Unguja.

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umekuwa na umuhimu na tija kwa jamii ya wasomi na wasiokuwa wasomi. Kwanza, utafiti huu unaweza kutumika kama maraejeo. Pili, utafiti unaweza

kuwaongoza watafiti kujua mapengo yanayoweza kujitokeza katika utafiti huu na wao kuyafanyia kazi. Tatu, utafiti huu unawezesha kuhifadhi amali za kiutamaduni zilizopo katika jamii. Nne, utafiti huu utasaidia watu kujua dhima ya matambiko jamii ya watu wa mkoa wa Kusini Unguja.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umekuwa na mipaka ya kitaaluma na mipaka ya kieneo. Katika mipaka ya kitaaluma utafiti umechambua dhima ya nyimbo za matambiko katika jamii ya watu wa mkoa wa Kusini Unguja. Kwa upande wa mipaka ya kieneo utafiti huu umefanyika Zanzibar katika kisiwa cha Unguja, mkoa wa Kusini, wilaya ya Kusini katika kijiji cha Makunduchi. Eneo hili limechaguliwa kwa sababu ni sehemu ya baadhi ya vijiji ambavyo bado vinaendeleza jadi hii ya matambiko, mtafiti alichagua eneo hili akitumai kuwa ni rahisi katika upatikanaji wa data zinazohitajika.

## 1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Utafiti huu umejumuisha sura kuu tano. Sura ya kwanza ni ya utangulizi ambayo imejikita katika usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja mpangilio wa utafiti.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, kwa kuangalia utangulizi, kazi tangulizi, pengo la maarifa na hitimisho.

Sura ya tatu imehusisha mbinu za utafiti. Vipengele vifuatavyo vimehusika, eneo la utafiti, kundi lengwa, ukusanyaji wa data za utafiti, sampuli na usampulishaji, data za utafiti, uchambuzi wa data, mbinu za uchambzi wa data, maadili ya utafiti na hitimisho.

Sura ya nne ni uwasilishaji, uchambuzi wa mjadala wa data za utafiti. Sura hii imehusisha uwasilishaji na uchambuzi wa maswali yautafiti kwa kurejelea nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe na Semiotiki. Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhtasari wa utafiti, mapendekezo na hitimisho.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imepitia kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti huu ili kupata maarifa yanayohusiana na mada ya utafiti. Vile vile, imegusia vipengele vya dhana ya nyimbo, aina ya nyimbo na nyimbo za matambiko, pamoja na nadharia zilizoongoza katika uwasilishaji na mjadala wa data. Kazi tangulizi zimesaidia kujenga uelewa wa mtafiti kuhusu maarifa yaliyofikiwa kwenye eneo la utafiti wake.

## 2.2 Maandiko Kuhusu Nyimbo

Hamadi na wenzake (1992) wanadai kwamba nyimbo ni mashairi mafupi ambayo hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Nyimbo zinaweza kuwa na ubeti mmoja na zaidi. Pia wanasema nyimbo hufungamana na utaratibu wa tungo za kishairi, na katika nyimbo zipo Sanaa za maghani na upigaji wa makofi.

Kipuri (2000) amesogea juu kabisa kwa kusema kuwa nyimbo lazima zitumike na zielezee falsafa ya maisha ya watu wa jamii husika, utamaduni wao, historia yao na maendeleo yao. Kwa vile nyimbo zinaeleza historia ya jamii ni dhahiri kuwa nyimbo za matambiko ni miongoni mwa nyimbo za kihistoaria zinazofafanua amali za kijamii. Kwa maana hiyo, kuonesha kuwa nyimbo zinabebwa na utamaduni wa jamii ni dhahihi uchunguzi wa nyimbo za matambiko za watu wa jamii ya Kusini Unguja ni jambo la msingi kwa sababu tumegun dua namna zinavyojeng ustawi wa jamii husika.

Katibula (1975) naye anasema nyimbo ni aina ya fasihi simulizi yenye namna pekee ya kujieleza, kila mtu huweza kuitumia bila ubaguzi kwa wakati wowote

anapojisikia. Anasisitiza kuwa nyimbo ni chombo cha kujifurahisha, kuonesha huzuni, kutoa mashambulizi na kuhami. Hata kama utafiti huu haukutazama nyimbo kwa mrengo aliofanya matafiti, bado inaonekana kuna umuhimu wa utafiti huo kwa sababu umeonesha njia ya kuwa nyimbo lazima ziwe na dhima pamoja na kusudi la yake.

Nkwera (1978) anasema nyimbo huwa ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Anafafanua maana ya muziki kwa kusema ni mpangilio wa sauti za ala na uimbaji unaoleta athari fulani kwa binadamu kupitia hisi zake na pia akili yake. Nkwera ameshatajwa anamalizia kwa kusema kuwa kilicho muhimu ni maneno ya uimbaji na sauti za ala, miondoko sio lazima. Maana ya nyimbo iliyotolewa na Nkwera yamemsaidia mtafiti kupata mwanga katika mada yake ya kuchunguza dhima za nyimbo za matambiko za jamii ya watu wa mkoa Kusini Unguja.

Mbarouk (1983) aliandika juu ya nyimbo za michezo ya watoto kisiwani Pemba na kusema kuwa kila jamii ya watu huwa na michezo yake ya jadi ambayo huchezwa na watoto wa jamii ile. Anaendelea kusema kuwa michezo hii mara nyingi huambatana na nyimbo. Katika kisiwa cha Pemba iko michezo mingi ya watoto nayo hutofautiana kila mtaa au pahala huwa na aina yake ya michezo ingawa mara nyengine michezo fulani inaweza ikaonekana kila mahali. Mbarouk (ameshatajwa) anaendelea kusema kuwa zikichunguzwa nyimbo zinazoimbwa katika michezo hii, nyingi zinaonekana hazina maana kamili, lakini huimbwa ili zilingane na mshindo na mpangilio wa michezo. Anamalizia kwa kusema kuwa ziko baadhi ya nyimbo ambazo zina maana kamili na kuwa zinatoa mafunzo fulani. Kinyume na makala ya Mbarouk ambaye amezungumzia nyimbo za michezo ya watoto kuwa ni aina nyingi.

Haji na wenzake (1992) wamefasili kuwa nyimbo ni mashairi mafupi hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Wameendelea kwa kusema nyimbo huwa ni fupi aghalabu huwa na ubeti mmoja tu wenye mistari mitatu. Nyimbo huweza kuambatana na sanaa ya kughani, ngoma, makofi au muziki. Watafiti hawa wametuonesha kuwa nyimbo zaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi jambo ambalo limempelekea mtafiti kuweza kuchunguza nyimbo za matambiko za watu wa jamii ya Kusini Unguja.

Njogu na Chimerah (1999) wameeleza kuwa nyimbo zinatokana na ushairi ambao ndio utanzu wa fasihi ulio mkongwe. Ambazo zilianzia na hisia za matukio yaliyowakuta watu katika miktadha na mandhari ya maisha yao ya raha na furaha, ugumu, kujituma, ama machungu na ushujaa. Anafafanua kwa kusema kwamba katika jamii za kilimwengu. Wimbo ulianza wakati binadamu alipobuni lugha, jambo ambalo lilimtoa mtu katika hali ya uhayawani na kumfanya kiumbe razini. Mabadiliko haya yalimfanya mtu ayaelewe mazingira yake na aweze kutoa mchango wake katika kuyakabili na kuyabadilisha mazingira hayo. Mawazo ya wataalamu hawa yatamuwezesha mtafiti kuyatumia na kuuendeleza utafiti huu ili kuweza kuchunguza dhima za nyimbo za matambiko za jamii ya watu wa mkoa Kusini Unguja jinsi zinavyotumika.

Wamitila (2003) anasema kuwa tungo za utanzu wa nyimbo zina mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha, na mapigo ya silabi ambayo hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki au wizani. Ingawa kanuni ya ala si ya lazima katika kuainisha

nyimbo, inawezekana wimbo ukaambatana na ala, kwa mfano chapuo, vugo, ngoma, marimba, pembe na zumari kwa sababu wimbo lazima uhusiane na ngoma.

Wamitila (ameshatajwa) ameelezea nyimbo kuwa lugha yake ya mkato na matumizi ya picha, mitindo hii vile vile inapatikana katika nyimbo za kubembelezea watoto hata kama nyimbo hizi hazina mapigo ya ala.

King'ei na Kisovi (2005) pia wamefasili nyimbo kuwa ni utungo wenye mpangilio maalum wa maneno na una mahadhi. Nyimbo huambatana na shughuli au jambo fulani, na sauti ya mwimbaji au waimbaji huwatia moyo watu kama vile wavuvi au wakulima katika kazi zao. Vile vile, nyimbo huimbwa kwa burudani katika sherehe kama vile harusi, ibada za kidini, kafara, matambiko na katika tohara za jando au unyago. King'ei na Kisovi wamesema nyimbo huambatana na shughuli au jambo fulani, mawazo haya yatamsaidia mtafiti katika kuchunguza dhima ya nyimbo katika matambiko ya jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja.

Asha (2018) anaeleza kuwa nyimbo ni aina ya ushairi iliyojaa usanii ndani yake inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu kwa maneno fasaha yenye muwala yenye kuleta taaswira, ishara, picha na sitiari iwe katika usemi au maandishi ili kuleta wazo au mawazo kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayoibua hisia kwa wahusika.

## 2.3 Tafiti Zilizofanywa Kuhusiana na Nyimbo

Thabit (2007) ameeandika tasnifu yake juu ya nafasi ya maudhui ya nyimbo za taarab katika jamii ya Zanzibar ya leo. Katika maandiko yake amesema kuwa nyimbo za taarab zinatoa maadili makubwa sana katika jamii husika lakini hakuishia

hapo amependekeza nyimbo nyengine zifanyiwe kazi katika vipengele vyengine ambavyo bado havijafanyiwa kazi. Utafiti wa Thabit umekuwa chachu ya kumpelekea mtafiti kuchunguza dhima za nyimbo za matambiko za jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja.

Salim (2009) alifanya utafiti kuhusiana na dhima ya nyimbo za daku kwa jamii ya Shehia ya Ole, wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Yeye ameeleza kuwa nyimbo za ngoma za daku bado jamii ya watu wengi hawajazingatia umuhimu wake. Licha ya kuwa nyimbo hizo zinaeleza dhima ya kuchunga, kukosoa na kurekebisha maadili ya jamii. Salim alieleza kuwa amegundua nyimbo za daku zina mwelekeo wa kotoweka, kwa vile watu wengi wa jamii ya Ole wanaonekana kuzipuuza na kuwavunja moyo waimbaji wa nyimbo hizo. Kazi hiyo ya Salim inaonekana kuwa na uhusiano na kazi hii ya utafiti, kwa vile amezungumzia dhima za nyimbo hizo jambo ambalo litamsaidia mtafititi wa utafiti huu katika kuchunguza dhima ya nyimbo za matambiko ya jamii ya watu wa mkoa Kusini Unguja katika jamii ya watu wa Makunduchi.

Sayfa (2007) alifanya uchunguzi kuhusu athari za nyimbo za harusi kwa mke na mume. Katika kazi yake alizungumzia kuhusu maisha ya ndoa Visiwani Zanzibar, alivyoona ni kuwa maisha ya ndoa yana mitazamo tafauti. Baadhi ya nyimbo za ndoa zimeonesha kuwa maisha ya ndoa ni suala la kubahatisha, wengine wameona kuwa ni nyenzo ya kuleta furaha na kuendeleza kizazi halali. Pia, ameeleza kuwa nyimbo hizo zinajenga athari kubwa katika kuitatulia jamii migogoro ya kindoa kama vile mke na mume kutoaminiana, kutuhumiana na kutovumilana.

Gora (2011) amefanya utafiti juu ya mitindo ya nyimbo za uganga wa pepo katika utafiti huu amegundua kwamba kuna msamiati wa kiganga unaotumika katika nyimbo za uganga. Utafiti huu umechunguza na kuchambua mitindo ya nyimbo za uganga wa pepo katika kufanya hivyo, kilichojitokeza ni kuwa utafiti uligundua kuwa nyimbo za uganga wa pepo katika kisiwa cha Kaskazini Unguja zina misamiati yake. Gora ameonesha na kugundua misamiati mbalimbali katika nyimbo za uganga wa pepo pamoja na mitindo inayotumiwa na waganga hao katika nyimbo za pepo. Kinyume na Gora utafiti huu umelenga kuchunguza dhima za nyimbo za matambiko za jamii ya watu wa mkoa Kusini Unguja katika jamii ya Makunduchi. Licha ya kuwa utafiti wake umenionesha njia tofauti katika kufikia mafanikio ya utafiti huu.

Mohamed (2014) katika tasnifu yake ameeleza kuhusu mchango wa nyimbo za ngoma ya Mdatu katika kudumisha maadili ya jamii ya watu wa Mafia. Maelezo yake yanaonesha kuwa nyimbo za Mdatu zina dhima kubwa katika jamii ikiwemo kuadilisha, kujenga uaminifu, kuwa na kauli nzuri katika ndoa, kuwaasa maharusi kuwa na matumizi mazuri ya fedha. Nyimbo hizo zimeelezwa kuwa nyimbo za Mdatu huimbwa katika shughuli za watu wa Mafia, kama harusi, unyago, posa, siasa na kilimo. (Na kila moja hubeba dhima ya kuelimisha na kuonesha umuhimu wake katika jamii). Katika utafiti huu umempa msukumo mtafiti katika kufanya kazi yake ya kuchunguza dhima za nyimbo za matambiko za jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja jinsi zinavyotumika katika jamii ya Makunduchi.

## 2.4 Maandiko Kuhusu Matambiko

Baraza la kiswahili la Zanzibar (BAKIZA, 2010) wanasema tambiko ni kitendo cha mtu au jamii kutekeleza ada maalumu kutuliza mashetani au mizimu. Matambiko

yamejengwa katika imani kuwa mababu waliofariki wana uwezo wa kuona matendo ya watoto na wajukuu wao walio hai. Inadhaniwa kuwa wanapokasirika watoto hupata matatizo ya magonjwa, vifo na mabalaa mengine. Ili kupoza hasira zao huko walikolala basi hupikwa pombe na vyakula vinavyokwenda kumwagwa makaburini au kuliwa na watu.

Kitula na Katherine (2010) wanasema neno matambiko linatokana na imani kuwa mababu waliofariki wana uwezo wa kuona matendo ya watoto wao waliohai. Inadhaniwa kuwa wanapokasirika watoto hupata matatizo ya magonjwa, vifo na mengine, ili kupoza hasira zao huko waliko lala. Hivyo, hupikwa pombe na vyakula vingine vinavyopendwa na kwenda kumwaga makaburini au kuliwa na waganga ambapo vitendo hivyo ndio matambiko.

Kamusi ya karne ya 21 (2011) wanasema, tambiko ni sadaka au ada inayotolewa kwa Mwenyezi Mungu pepo au mizimu moja kwa moja au kwa Mungu kupitia kwa miungu. Yapo matambiko yaliyotolewa na Wazee maarufu waliopewajukumu hilo. Matatizo yaliyoshindikana kwa mababu zetu yalipelekwa kwa Miungu ili iwasaidie kuyatatua.

Masebo (2008) anasema tambiko ni sadaka inayotolewa kwa Mwenyezi Mungu, Miungu au mahoka, mizimu na pepo kwao binafsi au kupitia kwa Mwenyezi Mungu wakati wa kusalia Miungu. Masebo anaendelea kusema kuwa matambiko yana umuhimu na hasara zake kwa jamii. Jamii hujenga imani kama ni chombo cha ktatulia matatizo. Pia, husaidia kuendeleza mila na desturi, huimarisha uhusiano miongoni mwa jamii. Kwa upande mwengine, matambiko hujenga dhana potofu

katika jamii kwa kuamini nguvu fulani bila na kuwa na uhakika wa kisayansi, husababisha ufukara miongoni mwa jamii kwa kufanya sadaka, kafara, huhitaji nyama, vyakula ambavyo hugharimu pesa nyingi.

Kasiga (2021) anazungumzia utaratibu wa matambiko yaliyofanywa na kabila la Waangavu waliopo nchini Tanzania. Katika tambiko hilo, ilimpasa kila mkuu wa ukoo kubaki na vazi alilopewa na Karima lenye manyoya ya aina mbalimbali ili kumtambulisha na kudhihirisha kuwa binadamu wana uhusiano wa karibu na manyani, komba, ngedere na masokwe. Hiyo, kila Mwangavu alijipaka rangi tafauti na ya mwenzake, rangi iliyompa utambulisho wa kipekee isiyoleta mfanano wowote na wenziwe ambao ungeweza kuleta matatizo katika matambiko ya Waangavu. Kwa kawaida tambiko la Waangavu husindikizwa na ulaji wa nyama mbichi ya mwanadamu ikiwa ni yamini ya kutohadithia lolote katika yote yaliyokuwa yanafanyika hapo. Mwishoni mwa tambiko hilo Waangavu huonesha umoja na mshikamano waliyoupanga. Andiko hili limemsaidia mtafiti kujua mbinu za kuyafanikisha matambiko ya aina mbalimbali yanayoambatana na nyimbo zake katika jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja. Hata hivyo, mtafiti amebaini mwachano wa kiutafiti. Hii ni kutokana na andiko lililopitiwa limezungumzia mchango wa matambiko kwa jamii ya Waangavu. Hivyo utafiti huu ulichunguza dhima ya nyimbo za matambiko katika jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja.

## 2.5 Tafiti Zilizofanywa Kuhusiana na Matambiko

Shemboko (2011) yeye alifanya utafiti kuhusiana na matambiko katika jamii ya wasambaa. Katika utafiti Shemboko aligundua kuwa Wasambaa hufanya tambiko katika sehemu toauti kama vile milima na miti mikubwa na hukutana kwa Wazee wa

mji pale linapotokea tatizo kwa ajili ya kuomba ili kutatuliwa shida zao. Kutokana na imani zao wanaamini kuwa shida zao nyingi hutatuka kwa kuomba kupitia matambiko. Kupitia utafiti huu umempa mwanga mtafiti wa utafiti huu ambao anaangalia dhima za nyimbo za matambiko katika kijiji cha Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja.

Olunga (2012) alifanya utafiti kuhusu ishara za mawasiliano katika matambiko katika jamii ya Wabukusu. Katika kuchunguza ishara hizo aligundua kuwa katika matambiko wahusika hutumia ishara maalumu katika mawasiliano jambo ambalo huathiri mwenendo wa ibada ya matambiko wakati watu wakiwasiliana kwa namna yao. Pia amegundua kuwa kuna lugha mbalimbali ambazo hutumika katika ibada hii ya matambiko. Utafiti huu umemsaidia mtafiti kujua lugha zinazotumika katika matambiko ambapo umemsaidia katika kuendeleza utafiti huu.

Mwaka Kogwa ni miongoni mwa matambiko yaliyoanza zamani na kuendelezwa huko Makunduchi Zanzibar. Toka zamani watu wa Makunduchi hufanya matambiko kwa kwenda kwenye mizimu ambayo ni mapango, miti mikubwa na makaburi ili kupata misaada ya mizimu hiyo. Muhando na Balisidya (1976) wanasema kuwa katika jamii ya asili watu walielekeza matatizo mbalimbali kwa Miungu yao ambayo kwa nguvu za kibinadamu yaliwashinda, walipopata tatizo ya ukame na mgonjwa ya hatari na vita walisali ili Miungu yao kuwasaidia. Hali ipo pia katika jamii ya watu wa jamii ya Kusini Unguja.

Mizimu ya makunduchi ni vibanda vidogovidogo, mapango na miti mikubwa. Mizimu hiyo huwekewavitambaa vyeupe, vyeusi na vyekundu. Mizimu maarufu

iliyohusishwa na matambiko ya Mwaka kogwa ni kijiwe pepo na kijiwe shomoo ambayo ipo Kusini Makunduchi. Mizimu ya mapopwe msikiti kichaka na mzimu wa kwa binti Khatibu ambayo ipo sehemu ya kati Makunduchi. Mizimu mengine ni ile ya mwanampabe, kipanga ngoma na mabuko ilioko kajengwa Makunduchi. Watu wa Makunduchi huenda kutambika kutokana na imani yao kubwa mizimu ina nguvu kubwa za ziada katika uendeshaji wa matatizo ya maisha yao.

Temples (1969) wabantu wanaamini kuwa mizimu ndio yenye ujuzi mwingi kuhusu maisha ya dunia. Ujuzi huu ndio unotumika kuendesha watu wasio hai au wafu. Matambiko ya watu wa Makunduchi hufanywa kutokana na sababu mbalimbali ambazo zipo nje ya uwezo wao, sababu hizo ni kama kupatwa na maradhi wasioweza kuyatibu, kukithiri kwa maovu kijijini mwao, kuombeana dua za mafanikio kujikinga na balaa pamoja na kuwashukuru wahenga na mizimu yao.

Swantirz (1970) alipofanya utafiti katika matambiko ya Waaramo aligundua aina tatu za Matambiko. Tambiko la kwanza ni lile linalohusu mambo ya kawaida ya maisha ya kila siku kama kuzliwa mtoto, kutahiriwa, kuvunja ungo wasichana, wanawake kupata ujauzito na matambiko ya mazishi. Aina ya pili ni matambiko yanayohusu imani za kiroho matambiko haya yanajumisha maombi na ibada mbalimbali zinazofanyika kwenye mizimu. Aina hii ya tatu ni matambiko yanayohusu matibabu ambayo hujumuisha kupata tiba ya kienyeji na kupata kinga mbalimbali ikiwmo kinga ya maradhi na majanga. Katika kijiji cha Makunduchi aina zote tatu za matambiko zimepewa nafasi kubwa.

Kila unapomalizika Mwaka na kukaribia kuanza Mwaka mpya watu wa Makunduchi hutambika tambiko la Mwaka Kogwa. Hutambika mizimu yao ili kuomba toba na

msamahha kutokana na maovu waliyofanya Mwaka mzima uliopita ili mizimu hiyo isije ikawadhuru. Ndio maana hata katika nyimbo wanasisitiza kwa ‘watoto wetu tunakupeni wosia, Mwaka mkiuacha mtaumia’

Khamis (2008) alibainisha kuwa imani za kutambika na kuamini mizimu ni jadi, zinazokwenda sambamba na utamaduni wa mswahili. Alibainisha kuwa matambiko mengi hufanyiwa mashetani katika maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kwani, hadi leo katika maeneo hayo vipo vibanda vya mizimu na matambiko ya Mwaka Kogwa. Andiko hili limemsaidia mtafiti kubaini uwepo wa mizimu na matambiko ya Mwaka Kogwa visiwani Unguja hali iliyomsaidia mtafiti kuchanguza ya Mkoa wa Kusini Unguja. Hata hivyo, andiko hili limeacha pengo la kiutafiti kwa sababu limezungumzia yanayofanywa visiwani kwa ujumla bila ya kugusia dhima za nyimbo za matambiko ya aina yoyote. Hivyo, utafiti huu ulichunguza dhima za nyimbo za matambiko ya jamii ya watu wa mkoa wa Kusini Unguja ili kujaza pengo lililoachwa wazi kutokana na pitio lililosomwa.

## 2.6 Nadharia ya Semiotiki

Nadharia inayoongoza katika uchambuzi wa data ni Semiotiki.  Semiotiki ni nadharia ya mfumo wa ishara na uashiriaji. Semiotiki ni neno linatokana na maneno ya Kiyunani semainon na semainomenon, yaani kitaja na kirejelee. Vitu hivi vinahusika zaidi na mfumo wa kanuni zinazotawala mila na desturi, na ambazo zinawezesha mambo ya kijamii na kiutamaduni yaonekane kama ishara (Holman na Harmon 1986 na Halliday, 1990). Msisitizo mkubwa wa nadharia hii ni kuchunguza kwa nini kazi za kifasihi zina maana zilizonazo kwa wasomaji wa kazi hizo (Wamitila 2003 :191).

Wanafalsafa Ferdinand de Saussure, Charles Pierce, Levi Strauss na wengine ndio wanaohusishwa na nadharia hii.

Pierce (1966: 99) kama alivyonukuliwa na Hill na Fenner (2010: 31), anafasili ishara au uwakilishi kama kitu kinachosimama badala ya kitu kingine. Anaamini kuwa, kila ishara inajengwa na kuundwa kwenye akili ya mtu ambapo binadamu hufikiri juu ya msingi na kategoria kwa kutumia alama, ambazo zinaweza kuwa sawa au zilizoendelea na kukua zaidi. Peirce anazigawa ishara hizi katika makundi mawili, yaani kitendwa (object) na kivumishi (modifier). Ishara hizi huwa katika maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na mtenda. Anaendelea kusema kuwa, kitu chochote kitakuwa na alama kama watu watakifasiri kama kirejelee kwamba kinasimama kwa niaba ya kitu kingine.

Ferdinand de Saussure kama alivyonukuliwa na Hill na Fenner (2010: 31) anaeleza kuwa nadharia ya Semiolojia huvichunguza na kuvibainisha vigezo vya ufasihi wa matini za kifasihi. Matini ambazo hutambuliwa kama za kifasihi katika jamii au tamaduni mbalimbali huonyesha sifa mbalimbali za kimuundo ambazo ni msingi mkuu wa utambuzi huo. Katika semiotiki kuna uhusiano kati ya muundo na maana. Barthes (1964) amezungumzia dhana ya msimbo ambao unahusu ishara na uashiriaji katika nadharia ya semiolojia. Lengo la Barthes ni kuivunja matini ya kifasihi kwenye sehemu ndogondogo alizoziita leksia. Kila leksia hudhihirisha misimbo na kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri matini ya kifasihi. Barthes aliainisha aina kuu tano za misimbo kama ifuatavyo:

**Msimbo wa Matukio:**

Msimbo huu unahusu jinsi matukio yanayopatikana katika hadithi au simulizi fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji au mtazamaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi yanavyofuatana ki-athari na ki-usababishi. Hivyo, kupitia msimbo huu mtafiti aliyaelezea matukio yanavyopatikana katika nyimbo za matambiko ya jamii ya watu wa mkoa Kusini Unguja jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wake kupitia nyimbo hizo za kifasihi. Pia mtafiti alielezea mshonano kutokana na kusababishana au kuathiriana kwa nyimbo hizo ili kuibua dhima za nyimbo hizo kupitia jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguj kwa kuangalia jinsi matukio yanavyofuatana kiathari kwa namna hiyo.

**Msimbo wa Kihemenitiki:**

Huu unahusu taharuki na simulizi au kutamba hadithi ambao unaweza kufumbatwa kwenye anwani ya kazi za kifasihi. Hivyo. Msimbo huu humfikirisha msomaji juu ya kile anachokikusudia kukisoma au kukitafiti. Utafiti huu uliongozwa na msimbo huu kutaka kujua kile kinachotakiwa kusimuliwa na wasanii ili kuzibainisha nyimbo za matambiko zilizopo katika jamii ya watu wa Makunduchi.

**Msimbo wa Kiseme:**

Neno *seme* hutumiwa kukielezea kipengele nasibishi cha kisemantiki. Hivi ni vipengele ambavyo vinatuwezesha kupata picha fulani. Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji au mtazamaji atakavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani wa kifasihi. Wamitila (2002) anaeleza kwamba neno sema hutumiwa kuelezea elementi nasibishi ya kisemantiki. Hizi ni elementi zinazomwezesha mtafiti kupata picha fulani kutokana na viashiria fulani kupelekea kujua sifa kamili za jambo, tukio, hali

au muhusika fulani wa kazi ya fasihi. Msimbo huu utasaidia kunasibisha baina ya vitu, watu, nyakati na hali zinazojitokeza katika kuzielezea nyimbo za matambiko ya jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja na kuhusisha na hali iliopo katika jamii ya Watanzania.

**Msimbo wa Kiishara:**

Huu ni msimbo muhimu katika usomaji au utazamaji na uhakiki wa kazi ya kifasihi. Msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji au watazamaji wanagundua maana za kiishara katika kazi ya kifasihi. Kupitia msimbo huu mtafiti alielezea na kugundua ishara zilizobebwa katika dhima za nyimbo za matambiko ya jamii ya watu wa mkoa wa Kusini Unguja. Ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Ili watu waelewe dhima za nyimbo zilizowasilishwa kupitia ishara fulani lazima watu hawa wawe na makubaliano fulani ambayo hutokana na kushiriki elimu, utamaduni, dini na mandhari sawa, watu kutoka jamii moja, wenye kuzungumza lugha moja na kushiriki utamaduni sawa huwa na ukubaliano kuhusu ishara fulani na maana zake ndani ya nyimbo za mkoa Kusini Unguja

**Msimbo wa Kirejelezi:**

Msimbo huu unajengwa kutokana na viashirii vya utamaduni vinavyorejelewa katika kazi ya fasihi inayohusika. Urejelezi huu huunda Uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu vinavyoeleweka na wasomaji au watazamaji, hivyo kuipa kazi ya kifasihi nguzo za kiutamaduni. Msomaji/ mtazamaji anaposema anaelewa akisemacho mtunzi huwa anasema hivi kutokana na viashirii vya msimbo huu.. Huhusisha matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji kwa kuipa kazi fulani nguzo za kiutamaduni. Msemaji anaposema kuwa anakielewa

kituanachokimaanisha msanii husema hivyo katika msingi wa kiurejelezi au kiutamaduni.Wamitila (2002) anasema kwamba urejelezi huu huunda Uhalisi mahsusi unaotokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo huipakazi fulani nguzo za kiutamaduni. Msimbo huu ulimsaidia mtafiti kugundua nyimbo za matambiko ya jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja

### 2.6.1 Mapungufu Yaliyobainika Katika Nadharia ya Simiontiki

Nadharia ya simiontiki imesaidia mno katika ukusanyaji na uchambuzi wa data lakini imeshindwa kusaidia katika lengo la pili la utafiti huu ambalo ni kuchunguza miktadha na maeneo ya utokeaji wa nyimbo za tambiko. Kwa hivyo, hii ndio sababu ya msingi ya kuongezea nadharia ya uhalisiajabu kwa sababu miktadha ya utokeaji na eneo linalotendeka tambiko litaweza kufafanuliwa kutokana na uajabu wa matukio yanayotendeka sehemu hiyo, hivyo, lengo hilo limekamilika na limeweza kupata data na kuchambuliwa kutokana na misingi ya uhaliajabu.

### 2.6.2 Nadharia ya Uhalisiamazingaumbwe

Uhalisiamazingaombwe kama dhana au istilahi umeanza katika miaka ya 1920. Shannin Schroeder anadai kwamba Mjerumani Franz Roh ndiye aliyevumbua na mtumiaji wa awali wa nadharia ya Uhalisi mazingaumbwe ambao ulijulikana kama 'Magischer Realismus' mnamo 1925 ambao ndio msingi wa 'Magical Realism' ya Kiingereza

Kwa mara ya kwanza Uhalisi mazingaumbwe haukutumika kuhakikia utanzu wa fasihi bali ilianza kuhakiki michoro na picha. D’Haen (2005) ameeleza kwa usahihi kwamba uhalisiamazingaombwe ni tawi mahsusi la usasabaadaye (postmodernism),

linaonesha sifa za usasabaadaye kama vile kujirejelearejelea, uziada uliopindukia, uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini.

Hata hivyo, hoja kwamba Roh ndiye mwasisi wa uhalisiamazingaombwe inapingwa au kurekebishwa na wahakiki kama vile Christopher Warnes anayedai kwamba matumizi ya awali kabisa ya istilahi ya 'uhalisiamazingaombwe' yanapatikana katika maandishi ya mshairi Friedrich Freiherr von Hardenberg, maarufu kwa lakabu ya kishairi Novalis, aliyezaliwa 1772 na kufariki kutokana na kifuakikuu 1801 akiwa na umri wa miaka 29.

Yumkini baadhi ya wataalam wanadai kuwa Novalis hakuikuza mno dhana ya uhalisiamazingaombwe pamoja na kwamba alikuwa wa kwanza kuitumia. Labda ndio sababu wengi humtaja Franz Roh aliyetumia kinadharia kauli ya uhalisiamazingaombwe

Njogu na Wafula (2007) wanasema kuwa uhalisia ajabu/ mazingaombwe ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelezwa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Katika Uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika (ya kifantasia) husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Dhana hii imeitazama fasihi kwa umbo la nje na sio kwa undani wake. Kwani fasihi inaweza kuwa na umbo la nje kwa macho ya kawaida lakini kwa undani wake Uhalisi ajabu hutumika ili kuwasilisha wazo la msingi la mwandishi. Walibora (2010) anashadidia ukweli huo kwa kusema, uhalisia mazingaombwe unapaswa kueleweka, kwa kadiri fulani, kama mkabala wa kuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka ya uhalisia.

**Misingi ya Uhalisi Mazingaumbwe**

a) Masimulizi yanawekwa sambamba na matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida. Katika msingi huu tunaona kwamba masimulizi ya kiajabuajabu yanayotokea ndio yale ambayo yanatokea pia katika uhalisia wa kawaida.

b) Uhalisia mazingaombwe unaafiki kutalii na kukaidi mipaka katika matumizi halisi ya jambo, si hoja kama mipaka hiyo ni ya kiontolojia, kisiasa, kijiografia au kiutanzu. Ni dhahiri kwamba baadhi ya mambo yanayotokea huwa si hali ya kawaida ukilinganisha na maisha halisi ya binaadamu.

c) Inakiuka sifa za uhalisia, katika mhimili katika masimulizi hujitokeza mambo ambayo ni kinyume na uhalisia ambayo kwa binadamu wa kawaida humpa dhana ambayo ni vigumu kuamini.

d) Matukio ya kuduwaza na kuogofya au kutisha ndio yanayoweza kueleza dhima ya fasihi, matukio mbalilmbali ambayo si kawaida ambayo hutokea kama vile kuzuka kwa upepo mkali, majitu yasio ya kawaida hubeba dhima na kuiwakilisha kwa jamii.

Katika kipengele cha uchambuzi wa data mtafiti anaamini kuwa nadharia hizi zitakidhi haja ya uchambuzi wa data zake kwa vile matukio mengi yanayotokea katika matambiko yanashabihiana na nadharia hii ya uhalisiaajabu kulingana na mada ya utafiti huu ya kuchunguza dhima ya nyimbo katika matambiko ya jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja.

## 2.7 Mkabala wa Nadharia ya Utafiti

Wafula na Njogu (2007) wanasema nadharia za uhakiki wa fasihi ni miongozo inayomsaidia msomaji wa kazi za fasihi kuifafanua kazi ile kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa vinavyozalika kutokana na uchunguzi wa aina mbali mbali za fasihi. (Eagleton 1983, Njogu na Chimela 1999) wanasema kuwa nadharia zinaweza kuchukuliwa kama jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya semiotiki na uhalisia mazingaombwe.

Mtafiti wa utafiti huu ameona ipo haja ya kutumia nadharia mbili kutokana na kuwa nadharia moja haijitoshelezi kwani kuna baadhi ya misingi haiwezi kufafanuliwa kwa kutumia nadharia ya uhalisia tu, kwani baadhi ya hoja ambazo ni za kutisha, kuogofya na kimaajabu ajabu, hoja hizi zinahitaji kufafanuliwa kwa kutumia misingi ya nadharia ya uhalisia mazingaombwe.

## 2.8 Pengo la Maarifa

Kutokana na kazi tangulizi zilizotafiti nyimbo za matambiko mtafiti amegundua kuwa nyimbo nyingi zimeangalia upande wa maudhui hasa katika upande wa nyimbo za taarabu za kisasa na za kizamani na bongo fleva. Mtafiti alibaini kuwa, tafiti nyingi hazikuonesha kipengele cha nyimbo za tamaduni jambo ambalo limemsukuma mtafiti wa utafiti huu kuchunguza dhima ya nyimbo katika matambiko katika kijiji cha Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja ili kuangalia maudhui yaliyomo kwenye nyimbo za matambiko zinaendana na uhalisia wa maisha. Pia kuangalia jadi hizi katika kijiji hichi cha Makunduchi zina msaada wowote kwa jamii kutatua shida zao baada ya maombi.

## 2.9 Hitimisho

Sura hii tuliangalia na kuchambua kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti huu. Pia ilimulika maandiko tangulizi yanayohusu nyimbo na matambiko. Vilevile kuangalia pengo la maarifa na mwisho kuangalia nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe na Semiotiki ambazo zitatumika katika utafiti huu na hitimisho la sura hii.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI NA VIFAA VYA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameeleza vipngele vinavyohusiana na sura hii kama vile eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanyia data, aina za data za utafiti, mbinu za uchambuzi wa data, mkabala wa uchambuzi wa data, zana au vifaa vya utafiti, maadili ya utafiti na hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni sehemu mojawapo muhimu katika utafiti, ni sehemu ambayo mtafiti huchagua mahali ambapo taarifa za mtafiti zimekusanywa. Utafiti huu ni wa uwandani ambao umekusanya data katika vyanzo tofauti vya watafitiwa. Utafiti huu utafanyika katika kisiwa cha Unguja, mkoa wa Kusini Unguja, Wilaya Kusini katika kijiji cha Makunduchi. Mtafiti huu amechagua eneo hili kwa kuwa walengwa jadi ya matambiko bado ipo katika kijiji teule hasa katika kipindi cha Mwaka Kogwa. Hivyo, anamini walengwa wamepatikana kwa urahisi.

## 3.3 Mbinu za Utafiti

Dawson (2002) anaeleza mbinu za utafiti ni njia zinazotumiwa na mtafiti katika ukusanyaji wa data kwa lengo la kuimarisha utafiti huo. Hivyo ili mtafiti aweze kufanya utafiti na kupata data za uhakika hanabudi kuteua mbinu zitakazomhakikishia anapata taarifa alizozikusudia kulingana na mada ya utafiti wake. Kulingana na utafiti huu mtafiti atatumia mbinu teule ambazo mtafiti ameziteua kulingana na mada ya utafiti wake.

### 3.4 Kundi Lengwa

Bryman (2004) anaeleza kuwa kundi lengwa ni jumla ya watu au vitu vyote vitakavyohusika katika utafiti. Hivyo kundi lengwa ni yale mambo yote ambayo yatanisaidia kupata data kutokana na maswali nitakayouliza. Hivyo kundi lengwa katika utafiti huu ni nyimbo za jadi ya matambiko katika kijijicha Makunduchi katika Mkoa wa Kusini Unguja.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwa kuwa si rahisi kutafiti kundi lengwa zima (Spata 2003, Briman 2004 na Waliman 2011) Uteuzi wa sampuli hii ulifanyika kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa. Hii ni mbinu ambayo mtafiti hutafuta sampuli ya watafitiwa kulingana na utafiti wake. Sampuli lengwa iliyotumika katika utafiti huu ni nyimbo za matambiko ya watu wa makunduchi na bwejuu tu. Katika utafiti huu Wazee 15 wenye tajriba ya matambiko walihojiwa, 10 miongoni mwao ni wanaume. Wanaume wameteuliwa wa wingi kwa sababu ndio washiriki wakuu wa matambiko ya watu wa Kusini unguja. Vijana 10, watano ni wanaume na watano ni wanawake.

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti wa kitaaluma mbinu za kukusanyia data zimegawika katika aina mbili.

#### 3.6.1 Data za Awali

Data za msingi ni data ambazo ni mpya kabisa ambazo hazijawahi kukusanywa na watafiti wote waliotangulia. Ni aina ya data ambazo mtafiti huzikusanya kwa

kutumia njia ya mahojiano, uchunguzi makini, maswali na majibu ya ana kwa ana . Hivyo data za utafiti huukupitia njia ya udodosaji, hojaji na ushuhudiaji makini.

### 3.6.2 Data za Upili

Kamuzora na Adam (2008) wanasema, Data za upili ni data zote zinazopatikana kutoka vyanzo tangulizi au data zilizokusanywa na watu wengine kwa malengo maalumu. Katika utafiti huudata za upili kwa kusoma Makala, majarida, wavuti, vitabu na marejeleo mengineyo ambayo yatatilia mkazo maeneo ambayo yataendana na utafiti huu.

## 3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Dawson (2002) anafasili dhana ya mbinu za utafiti kuwa ni zana au njia zinazotumiwa na mtafiti katika ukusanyaji wa data. Mtafiti wa utafiti huu ametumia mbinu ya masikanini (makaazini), mbinu ya usaili na mbinu ya mahojiano akiamini kuwa mbinu hizi zimempa taarifa za kutosha katika kupambanua kulingana na mada yake.

### 3.7.1 Mbinu ya Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni mbinu ya kisayansi ya kukusanyia data za utafiti. Kothari (2004:96) anaeleza kuwa mtafiti kama ataipangilia vizuri mbinu hii kwa kuzingatia malengo ya utafiti hudhibiti ukweli na uhalisia wa data za utafiti. Kwa kupitia mbinu hii mtafiti anakwenda moja kwa moja katika eneo la husika kushuhudia tendo linalofanyika na kukusanya taarifa anazozihitaji juu ya jambo hilo. Katika utafiti huu mtafiti alishuhudia baadhi ya matambiko mchache kwani jadi hii imeanza kutoweka kwa kasi kwa mujibu wa wanakijiji hao. Kushuhudia huko kumemsaidia mtafiti kupata

taarifa alizohitaji kwa kuona yeye mwenyewe baadhi ya matukio yalivyofanyika jambo ambalo lilimpa mwanga wa kufikia malengo utafiti huu.

### 3.7.2 Mbinu za Usaili

Usaili ni mpangilio mzima wa mfano wa maswali yenye lengo la kutafuta data au taarifa kwa njia ya mazngumzo ya ana kwa ana kwa kutumia maswali ya mitindo tofauti tofauti, (Kothari, 2009). Mtafiti aliandaa maswali yaliyomuongoza katika usaili huo. Kupitia mbinu hii mtafiti ameandaa usaili na watafitiwa wengine wakiwemo wa nyimbo za matambiko katika kijiji cha Makunduchi. Mtafiti ametumia mbinu hii kwa wasailiwa wanaojua na wasiojua kusoma. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya nyimbo na katika kupata data nyengine za uhakika kutoka kwa walengwa jambo ambalo lilisababisha mtafiti kuyafikia malengo ya utafiti huu kuhusu dhima ya nyimbo za matambiko katika kijiji cha Makunduchi.

## 3.8 Uchambuzi wa Data

Kothari (2004) anasema kuwa baada ya kukusanya data inampasa mtafiti kuzichakata na kuzichambua kwa kurejelea malengo ya utafiti. Mtafiti wa utafiti huu ametumia mbinu mkabala wa kimaelezo katika kuchambua data zake. Kothar (1990) anaeleza kuwa, mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na malengo ya utafiti wake.

Vilevile katika uchambuzi wa data mtafiti amezingatia matumizi ya nadharia husika katika kuhusisha mada, malengo na mswali ya utafiti. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Semiotiki na uhalisia mazingaombwe ndizo zilizotumika

kuchanganua data za utafiti huu ambayo mtafiti ameona kuwa ni muafaka zaidi katika kulingana na malengo ya utafiti wake ambapo nadharia moja imesaidia pale ambapo nadharia moja haikukidhi haja ya utafiti huu.

## 3.9 Usahihi wa Utafiti

Kwa nia safi, mtafiti anaamini kwamba data zote zilizokusanywa zimekuwa sahihi na za uhakika hii ni kutokana na sababu mbalimbali. Kwanza mtafiti alipitia nyaraka tofauti kama vile majarida, makala mbalimbali, pamoja na kukusanya data na kuzifanyia uchambuzi yakinifu na uhakika huku akiamini kwamba data hizo zimemsaidia vya kutosha katika kutoa majibu sahihi ya maswali yake ya utafiti.

Pili, mtafiti amepitia mitandao kupataq taarifa zaidi, kusikiliza vyombo vya habari kama redio kulingana na mada yake inayohusiana na matambiko ambapo amepata maarifa na data zinazohusiana na mada yake ambavyo zimesaidia vyakutosha katika utafiti huu.

Mwisho, mtafiti ana imani kupata fursa muhimu na adhimu ya kupitiwa na kusomwa kwa utafiti huu na msimamizi kumempa fursa na uweledi wa kupanua mawazo kitaaluma kwa kuweza kukamilisha utafiti huu kwa kufuata maelekezo aliyopewa na kurekebisha kasoro zilizopo ndani ya utafiti huu.

## 3.10 Maadili ya Utafiti

Linasema, Maadili ya utafiti yanahusu matumizi mazuri, kanuni bora, uadilifu kwa mtafiti na watafitiwa na katika mada yenyewe. Kuna masuala mengi ya kimaadili ambayo yanahitaji kutiliwa maanani katika utafiti, moja kulinda usalama, uaminifu, kujuwa majukumu ya watafitiwa na nidhamu bora ya kazi.

Seture (2010) anaeleza mkabala wa maadili ni moja wapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti alipaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati, akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Mtafiti wa utafiti huu amezitambua haki zote na kuzifanyia kazi pamoja na kuzingatia silka, kutekeleza maadili, kanuni na taratibu stahiki za kiutafiti ili kuhakikisha ukusanyaji wa data umekuwa sahihi na uhakika katika kujibu maswali ya utafiti huu.

## 3.11 Zana na Vifaa vya Utafiti

anaeleza, vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, lakini aghlabu baadhi ya vifaa hivyo huwa ni pamoja na kalamu, penseli, shajara, tepu rikoda, kamera kompyuta,. Hivyo mtafiti analazimika, kutumia vifaa vitakavyoendana na mahitaji ya ukusanyaji wa data. Vifaa hivyo hutumika kwa lengo la kuweka kumbukumbu za utafiti.

### 3.11.1 Kompyuta

Kompyuta ni kifaa kilichotumika katika kuchapa tasnifu hii tokea mwanzo hadi mwisho. Kompyuta pia imetumika katika kutafuta nukuu mbalimbali mtandaoni zinazohusiana na utafiti huu.

### 3.11.2 Kalamu na Karatasi

Kalamu na karatasi zimetumika pia katika katika kunukuu taarifa mbalimbali kutoka kwa watafitiwa. Vifaa ni muhimu katika utafiti huu kwani ni rahisi na vinabebeka pahala popote mtafiti akiamini kuwa zana hizi zimekuwa na tija katika kukusanya kumbukumbu iwapo zitahifadhiwa kwa makini.

## 3.12 Muhtasari

Sura hii iliangazia mbinu za utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanyia data, aina za data za utafiti, mbinu za uchambuzi wa data, mkabala wa uchambuzi wa data, usahihi wa utafiti, maadili ya utafiti zana au vifaa vya utafiti, na hitimisho.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data. Katika sura hii data zilizokusanywa na mtafiti zimefanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Ni katika sura hii ambapo maswali ya utafiti yamepatiwa majibu yake. Uwasilishaji data umepangwa kutegemea malengo mahsusi. Mtafiti amewasilisha, kuchambua na kujadili data zinazohusu nyimbo za matambiko zilizopo katika jamii ya watu wa Makunduchi, mahali, wakati na jinsi nyimbo zinavyotumika pamoja na kuchunguza dhima na mchango wa nyimbo za matambiko katika jamii ya watu wa Mkoa wa Kusini Unguja. Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo katika utafiti huu umepangwa katika mtiririko wa kufuata malengo mahsusi.

## 4.2 Nyimbo za Matambiko Zilizopo katika Jamii ya Watu wa Makunduchi.

Sehemu hii imefafanua lengo la kwanza la utafiti. Kwa kubainisha nyimbo mbalimbali za tambiko zinazopatikana katika jamii ya watu wa Kusini Unguja. Katika jamii ya wamekunduchi tumebaini kuwa nyimbo za matambiko huimbwa kwa kutegemea amali na dhima ya wakati husika. Nyimbo hizo zinaweza kuwa za ufunguzi wa matambiko, nyimbo zinazoimbwa kuondoa mikasa, Wimbo wa kuomba mvua, kufukuza magonjwa, kushukuru, ukaribishaji wa wageni na ufungaji wa matambiko.

### 4.2.1 Wimbo wa Kuingia Matambikoni

Katika tambiko kunaweza kuimbwa nyimbo wakati kwa kufanya ibada katika tambiko husika. Utafiti huu umebaini kuwa zipo nyimbo za kuomba ruhusa ya kufika

au kuingia katika mzimu au sehemu inayokusudiwa kufanyika tambiko hilo. Nyimbo hizo huimbwa kwa kuomba ruhusa kwa kutumia neno hodi. Mtambikaji anapoingia katika sehemu ya matambiko (mzimuni) huwa na utaratibu maalumu unaomuongoza mtambikaji kuingia ndani. Mtambikaji hulazimika kubisha hodi kama afanyavyo wakati wa kuingia nyumbani hodi hii huwainayomtambulisha kama yeye ni mwanachama hai katika kilinge husika. Mtambikaji hutegemea aina ya tambiko analotaka kulifanya. Wakati hutakiwa apige hodi hali ya kwenda kinyumenyume huku akiimba wimbo huo. Mfano wa wimbo unaonekana kwenye jedweli namba 1 hapo chini

**Jedweli Namba 1: Wimbo wa Kuomba Ruhusa ya Kuingia Katika Tambiko**

| **Wimbo kwa lahaja ya Kimakunduchi** | **Tafsiri ya Wimbo kwa kiswahili sanifu** |
|---|---|
| hodi tunangia hodi x2 Enyi wakuu wa<br>tambiko x2<br>Tunakuja suye hodi wanenu hodi x2<br>Mutupokele kwa mikono yenu hodi x2<br>Mutukubaliye tunayoyajisa kwenu hodi,<br>uno ukenja tunaupiga kwenu<br>hodiTunagia kilingeni nyuye! Hodi x2<br>Wakuu wa kula pembe, kaskazi ino yenu<br>sadaka hodi x2 Na wale wa uchwejua,<br>ino sadaka yenu urejua na kusii hodi x2<br>Suye suye wanakele suye nyiye hodi x2<br>Tunangia ulingoni suye hodi x2 | Hodi hodi tunaingiax2 Wakuu wa<br>tambiko<br>Tunakusa siye, watoto wenu, mtupokee<br>kwa mikono yenu hodix2<br>Mkubali tunayoyaleta, kwenu tunatoa<br>sauti/ kelele muisikie, hodi<br>Wakuu wa kila pahali, wa Kasikazini hii<br>sadaka yenu, wa Magharibi hii sadaka<br>yenu, wamashariki hii sadaka yenu na<br>Kusini hodi<br>Sie watoto wenu tunaomba ruhusa ya<br>kuingia |

(**Mwimbaji**, Ali, 2020)

Mwimbaji anapofika katika ya wimbo huo wa tambiko hutokea ndege jamii ya popo na kupita juu ya kichwa chake. Popo hao humzidishia hamasa mtambikaji na kuendelea kuuimba wimbo huo kwa sauti nzuri kwa sababu huwa ni ishara ya kukubaliwa kuingia katika mzimu na akikaribia sehemu ya tambiko hukaribishwa na sauti yenye ukelele mkubwa kutoka ndani ya mzimuni bila ya kuonekana aliyeupiga ukelele huo. Hiyo huwa ni ishara na hiyo huwa dalili ya kukaribishwa mzimuni kwa mara ya pili. Nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe kupitia muhimili wa masimulizi yanawekwa sambamba na matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida, msingi huu imemsadia mtafiti kugundua mwimbaji anapouimba wimbo wa kuingia katika matambiko hutokea majini wanaojitokeza katika umbo la ndege aina ya popo wanaoruka angani katika hali ya kiajabuajabu iliyozoeleka na watambikaji. Hali hiyo hufanana na ile inayotokea katika uhalisia wa maisha ya kawaida unaomwezesha mtambikaji kutekeleza matambiko ya aina mbalimbali aliyoyakusudia.

### 4.2.2 Kuwakaribisha Wageni

Mwimbo mwingine ulibainika katika tambiko ni ule wa kukaribisha wageni waliodhamiria kuangalia au kuomba. Kwa kawaida, matambiko ya Kusini Unguja hutumiwa na mwenyeji na wageni. Ikitokea mgeni anataka kutumia tambiko hilo mwana kiringe huimba wimbo wa kuwakaribisha wageni hao. Ukaribishaji huu huwa unalenga kuwaombea ruhusa kwa mizimu ili wasije wakadhurika.

Wageni na wenyeji wanapofika katika matambiko hukusanyika na kukaa katika sehemu inayofanywa matambiko. Mara baada ya kuwasili wote huimbwa wimbo wa kuwakaribisha wageni wote waliohudhuria katika matambiko hayo. Kiongozi wa matambiko hutoa ishara ya kuwaruhusu waimbaji wa wimbo wa kuwakaribisha

wageni na wenyeji kutoka sehemu mbalimbali kwa lengo la kuhudhuria na kufanikisha matambiko husika. Wimbo unaoimbwa matoka makaribisho hayo ni huu ufuatao:

Wimbo wa Karibu mgeni
Karibuni wageni wetu jauno njo ucheza kwetux 2
Wageni wentu karibuni nyie karibuni x2
Kuja kutenbea kwetu ohoo! Kwetu x2
Kunadumisha undugu ohoo! Undugu x2
Nyoti karibuni nyiee karibuni x2
Wa kusi na Kaskazi nyoti karibuni x2
Wa uchwejua na urejua nanyi sogeani
Wa nchi jirani na wa mbali karibuni x2
Jihisini muwa huru kwetu x2
Pano matambikoni ohoo! Karibuni x2
Nayi Wakuyu nyote Wakuyu karibuni x2
Njo pano petu pano petu x2
Tutendape matambiko yano manufaa x2
Karibuni nyoti karibuni x2
Pano matambikoni kwetu nyiee karibunix2
Enyi mizimu musiwazuru wano wageni x2
Warudi makwao ee makwao x2
Kwa salama na amanix2
Nyoti karibunix2
(**Mwimbaji**, Hassani, 2020)
Kiitikio
Twawapokea nyoti twawapokea x2

Katika wimbo huu kipo kipnde kinachoamba mizimu isiye kuwadhuru wageni waliohudhuria. Hii ni ishara ya kuwa mizimu hii inadhuru na inanufaisha kwa mujibu wa itikadi ya Waswahili wa Kusini Unguja. Ushahidi wa hayo Ni Mwimbo Wa Karibu Mgeni pale aliposema

Mwimbo wa Karibu Mgeni

Pano matambikoni kwetu nyiee karibunix2

“Enyi mizimu musiwazuru wano wageni x2

Warudi makwao ee makwao x2

Kwa salama na amanix2 Nyoti karibunix2”.

Kwa mujibu wa msimbo wa utamaduni wa nadharia ya simiontiki kuwa ni wazi fasihi ya jamii huwa inalenga kufafanua falsafa za kiutamaduni za jamii husika. Aidha katika nadharia ya uhalisiajabu nayo inaonesha wazi kuwa fasihi na sanaa za waswahili zinaweza kuwa na uAajabu na Uhalisi kwa sababu zinatumia matendo na mambo ya ajabu lakini yanaaminiwa kutokea kwake. Pale mwimbaji anaposema msiwadhuru huwa hakuna kiumbe kinachoonekana lakini sauti iliyotoka huwa ni ishara ya kukubaliana na mizimu hiyo.

### 4.2.3 Wimbo wa Kuomba Mvua

Mwimbo mwingine unaojitokeza katika matambiko ya watu wa Kusini ni ule wa kuomba mvua. Jamii ya watu wa Kusini Unguja kufanya maombi katika mizimu kila wanapopatwa na tatizo. Hivyo, ikitokea kuadimika kwa mvua huandaa mizimu kwa ajili ya kufanya maombi. Wimbo unaimbwa katika shughuli hiyo ni:-

| **Wimbo ulioimbwa kwa lugha ya Kimakunduchi** | **Tafsiri ya Wimbo** |
|---|---|
| Machozi yanadondoka yoneni enyi wasifika ee x2<br>vulya imakatika kwenu tunaelekea ee x2<br>Twakuombani wakuyu nwasadaka twatoa x2<br>Damu tunajitolea ng’ombe kuwachinjia x2<br>Tunyedheeni vulya neema ituingiye ee x2<br>Hima hima kwenu shime  maombi tawaletea ee x2<br>Ya vulya tunayaleta suyemtunyeshezee ee x2<br>Mkono tunainua vulya tugaieni enyi mahoka x2 | Machozi yanadondoka yaoneni enyi wasifika ee x2<br>Mvua imakatika kwenu tunaelekea ee x2<br>Twakuombeni wakuu na sadaka twatoa x2<br>Damu tunajitolea ng’ombe kuwachinjia x2<br>Itunyeshee vua neema ituingiye ee x2<br>Hima hima kwenu shime  maombi tawaletea ee x2<br>Ya vua tunayaleta suyemtunyeshezee ee x2<br>Mkono tunainua mvua tugaieni enyi mahoka x2 |

(Mwimbaji, Khalidi, 2020)

Kwa mujibu wa nadharia ya Simiontiki katika msimbo wa utambaduni unaobainisha kwa kazi ya fasihi lazima iendane na utamaduni wa jamii. Hii ni dhahiri kuwa tambiko ni miongoni mwa utamaduni wa watu wa Kusini unguja. Hivyo nadharia hii imesadifu kubainisha tamaduni za jamii. Aidha, katika wimbo huu unafafanulia tena na nadharia ya uhalisiajabu katika msingi wa matumizi ya viumbe wa ajabu kama vile mashetani. Katika maelezo ya kuomba mvua wanaoelekewa katika maombi haya ni shetani. Kwa mfano, ndani ya ubeti huu shetani anatajwa kwa jina lake “mahoka” mahoka ni miongoni mwa shetani wanoaminiwa na watu wa Kusini Unguja kuwa na uwezo wa kutatua shida zinazowakabili.

### 4.2.4 Wimbo wa Kuombewa Ulinzi na Amani Kwa Wanandoa

Wimbo mwingine uliobainika katika utafiti huu ni ule wa kuomba baraka kwa wana ndoa. Mizimu hii imekuwa ikitumika kuomba kila jambo analohitaji msaada mwanadamu. Kwa jamii ya Wamakunduchi wanandoa walio katika kilinge hupelekwa mzimuni baada ya ndoa yao na kuombewa baraka pamoja na kukabidhiwa kwa mizimu ili kupata ulinzi kutokana na shari za wanadamu majini. Mfano wa wimbo uliobainika ni

Wimbo wa Malezi ya mtoto,
Tumemleta mwana mkadiid sana,
Mumfunze vyema walimwengu kumuona,
Mumdhibiti sana na mumlole vyema,
Ooo mabwana kazi muifanye vyema,
Ugovi wa ndoa/misikosuko katika ndoa,
Raha ziondoko zote moyoni,
Mengio masumbuko yalo nyumbani,
Mazuri yote yatoko kuchakutwa shetani,
Twayakabidhi kwako eye mukenga yetu ya moyoni x2.

Nadharia ya Uhalisiajabu ndio inayotuongoza kuona kuwa katika falsafa za afrika majini na misimu ni uhali wa maisha ya watu. Mizimu inaweza kutumiwa kama baraka kutoka kwa wazazi waliotangulia kuzimu. Kwa sababu mizimu sio shetani tu bali hata roho za ndugu waliotangulia zinaweza kuishi na kujumuika katika ulimwengu wa roho za wanadamu na ndio maana roho hizo hupewa uwezo wa kutatua matatizo ya wana jamii.

### 4.2.5 Mwimbo wa Kuomba Kupata Mtoto

Wimbo mwingine ni ule wa kuomba kupata mtoto. Wimbo huu hufanyika kama maombi au sala maalumu kwa mwanadoa. Miongoni mwa hazini ya muafrika ni uona anapata mtotot baada ya ndoa. Mtoto katika jamii za afrika hutazamwa kama falsafa ya utajiri au utatuzi wa migogoro. Hivyo, muafrika anapokosa mtoto hujitahidi kuomba na kufanya jitihada za kila aina ili aweze kupata mtoto huo

Wimbo wa muomba moto
Nija omba Mtoto
Siku zimenda mimba zamwagika
Twahitaji kinda nasi kutajika
Leo tutashinda yano vano mpaka kucha
Eee mwanamtamu nasi twamchaka
Kuepushwa na mabalaa/mikosi

Sala hii ya kuomba mtoto hufanywa wakati mwanadoa aliopata miaka miwili au zaidi bila ya kupata mtoto. Maombi haya yanaelekezwa kwa kuonesha msisitizo kuwa mimba zinazopatikana hazitungi na badala yake zinaporomoka na kumwangika (kuharibika). Maombi haya yanaelekezwa moja kwa moja kwa mizimu. Jambo ambalo ni imani ya halisi katika jamii za Waafrika lakini inaonekanakama ajabu kwa watu wasiokuwa na ambali hii. Hivyo ni wazi kuwa nadharia ya Uhalisi ajabu imesibu kutuonesha kuwa viumbe wa ajabu na wale wa kidhahania wanatumika katika sanaa na fasihi za waafrika. Magdalena na Chinemerem (2021) wanasisitiza kuwa tambiko ni moja ya amali za mwanadamu zinazomlea tangu utotoni hadi kufa kwake. Hivyo, tambiko linaweza kufanywa tangu mtoto aliyeko tumboni, maisha ya

kila siku n ahata muda wa kifo chake. Kwa mujibu wa maelezo hayo, ni wazi kuwa tambiko linaweza kufanywa wakati wa kuomba mtoto kama tulivyogundua katika utafiti huu.

### 4.2.6 Wimbo wa Kuomba Neema na Baraka

Katika shughuli za kijamii; binaadamu huwa anamahitaji yake katika shughuli za maisha ya kila siku kama vile kilimo, uvuvi na biashara. Utafiti huu umegundua matambiko ya Kusini Unguja hutumika kuomba baraka na neema katika shughuli wazifanyazo. Wimbo ufuatao ni ushahidi unaoonesha matambiko ya watu wa Kusini yanavyowezesha kuzifikia amali za kijamii.

Mwimbo wa njaa kali
Hapo awali miji ulikuwa mwanana,
Sasa njaa kali jua lawaka sana,
Mabalaa mbalimbali yawakumba wana,
Wavyele na rijali sote twasokotana,
Twawaombe mwabwana x2,
Kazi hii muitulize vyema x2,
Hapo awali miji ulikuwa mwanana,
Sasa njaa kali jua lawaka sana,
Mabalaa mbalimbali yawakumba wana.
wavyele na rijali sote twasokotana
twawaombe mwabwana x2
kazi hii muitulize vyema x2

Utafiti umegundua kuwa wimbo huu unaimbwa wakati wa kuomba neema baada ya majanga ya uhaba wa nafaka, njaaau hata ukosefu wa mvua. Dua hizi ziliimbwa samba na kutoa sadaka kwa mizimu. Neno “mabwana” nimetumika kuitukuza miungu au mizimu. katika ubeti huu mizimu inaelezwa shida walizonazo wana jamii, balaa au dhiki. Adamson (2012) Waafrika wanaamini miungu ya jadi kuwa na nguvu kuliko miuungu iliyofundishwa kutoka katika mafundisho ya wageni kama vile waarabu na wazungu. Miungu hao ni wema sana na wanapokea dua kwa haraka, ni miungu wenye kutoa baraka na neema kwa wanadamu bila kuwa na choyo. Kabla ujio wa Wakoloni Waafrika waliomba na kuabudu na walifanikiwa katika maombi yao, mifugo yao iliongezeka na mashamba yao yalinawiwri kutokana na baraka za miuungu hao.

### 4.2.7 Mwimbo wa Kufukuza Ugonjwa na Kuomba Afya Njema

Utafiti huu umebaini kuwa zipo nyimbo ziimbwazo kwa lengo la kuomba ufua ya afya. Ikitokea Makunduchi kupata maradhi tofauti ambayo hupelekea udhaifu wa mwili dua za kuomba kurudishiwa afya hufanyika kwa utaratibu wa kuimba. tiba hizo hufanyika sehemu zenye mizimu na jadi za wanajamii kama vile katika mapango na miti mikubwa. Kwa mfano muwele akifikishwa katika eneo hilo huimba wimbo ufuatao:

Mwimbo wa Mbatatao,
kuno kukonda njonini mbatatao maungo yaje,
Uno mbatatao homa gani maungo yaje,
Uno mbatato shetani gani maungo yaje,

Huo ni wmbo ambao wananchi huomba kurejeshewa maungo yao kutokana na kuumwa na maradhi mbalimbali na miili yao kudhoofu. Neno mbatatao nimetumika kama jina la mzimu, Mungu au shetani wanaamini kuleta afya na afuwa ya mwili pale unaposibiwa na maradhi. Katika kila stari mbatatao anatajwa kwa lengo la kuomboleza na kumtuza.

### 4.2.8 Wimbo wa Ufunguzi wa Pungwa

Pungwa ni ngoma ya mashetani inayotumika kulinda mji na familia. Ngoma hii hupigwa kila Mwaka kwa lengo la kutafuta usalama wa mji. Hata hivyo, pungwa inaweza kupigwa na wana kiringe au wamiliki wa mashetani kwa lengo la kutibia wagonjwa au kutibu majanga yanayotokeza katika jamii. Wakati wa kupingwa kwa ngoma hii mwanandege au mwana kiringe mwenye shetani ya pungwa huchagawa popote alipo hata awe kwenye masafa makubwa ya kijiografia pindi tu ngoma hii inapopingwa.

Wimbo wa mwenye mtoto atowe
Pungwa,
Pungwa watotoe ee,
Mwenye mtoto aondoshe,
Pungwa watoto ee,
Ng’ombe yule nitoe.

Wimbo huu huimbwa wakati wa usiku, nyimbo hii huimbwa na watu wazima na hawatakiwi kuwepo watoto kwa sababa shetani wa ngoma hii, anaweza kumsibu mtu yeyote atakaye kuwapo wakati ngoma ikipigwa. Kwa maana hii ngoma hapigwi mbele wa watoto. Hivyo, pale inapoanza kupigwa ni lazima itolewe tahadhari wa

wale walioleta watoto wao. Nyimbo hizi huimbwa kama burudani na kupeana faraja kutokana na shida na mahangaiko ya mchana kutwa.

### 4.2.9 Wimbo wa Kumtambika Mtoto

Katika jamii ya watu wa Kusini hufanyika tambiko la baada yam ja mzito kujifungua salama. Mtoto huyo hufanyiwa ada za kukabidhiwa kwa Wazee yaani shetani wanaotumika kulinda mtoto. Katika tambiko hilo huchinjwa kuku na kupikwa chakula kwa ajili ya sadaka. Wimbo mashuhuri uimbwao wakati huo ni

Wimbo wa singarimbwa

Singaribwa singaribwa,

Singaribwa, vyema kuvyalya,

Singarimbwa.

Wimbo huu huibwa kwa lengo la kutambulisha kuwa mtoto mwema amezaliwa katika kijiji hicho. Utamaduni huu wa kumfanyia mtoto tambiko umezoeleka katika miji mingi Afrika. Eberhard-Gran, (2010) anaeleza kuwa, katika jamii ya Ibo-Nigeria hufanyika tambiko baada ya mama mja mzito kujifungua salama tambiko hilo hufanywa kwa ajili ya kushukuru na kumtukuza kiumbe mpya aliyekuja ulimwenguni. Matambiko hayo hayaanzi kwa mama kujifungua bali huanza tangu mama akianza kubeba mimba.

## 4.3 Mahali, Wakati na Jinsi Nyimbo Zinavyotumika katika Mkoa wa Kusini Unguja

Sehemu hii itafafanua lengo la pili la utafiti ambalo ni kufafanua mahali, wakati na jinsi nyimbo za tambiko zinavyoimbwa katika mkoa wa Kusini Unguja. Kutokana na

imani ya watu wa Makunduchi na Bwejuu nyimbo hizi haziimbwi ovyoovyo tu bali huimbwa kutokana na wakati na sehemu maalumu. Utafiti huu umebaini maeneo, wakati na jinsi matambiko hayo yanavyofanyika kama itakavyofafanuliwa hapo chini.

### 4.4 Matambiko Yanayofanyika Pwani

Utafiti umebaini matambiko mengi ya watu wa Kusini hufanyika pwani. Wakati wa maji yakiwa yamejaa au kupwa. Mara nyingi hufanyika muda wa asubuhi mapema au juu likiwa linazama. Wakati huu unaaminika kuwa ni muda wenye baraka. Matambiko yanayofanyika Pwani huwa yanalenga utabiri wa maradhi na tiba ya maradhi hayo pindi yatakao tokezea. Utabiri ni ubashiri wa mambo yatakayotokea baadae ( BAKIZA, 2010). Wakati wa utabiri nyimbo maalumu huimbwa kwa lengo la kueleza shida zilipo kijijini. Wazee na wahusika wa matambiko ndipo wanapochukua fursa ya kwenda Pwani wakati wa alfajiri na kuangalia mapambazuko ya alfajiri ndipo wanapogundua hali fulani na kutabiri juu ya shida zinazoikabili jamii wimbo ufuatao huibwa katika tukio hilo.

Mwimbo wa mwana kidete

Mwana kidete,

Mwaka na mwana kidete mnasemaje,

Laila Pwani kuja udagaa na usitende.

Mwimbo huu huimbwa kwa sauti ya huzuni na kuashiria kama maombi ya kutekelezewa shida zilizowakabili wanajamii. Hivyo, baharini ni sehemu tukufu kwa wanajamii wa makunduchi na ndio maana baadhia ya matambiko yao yakafanyika hapo kwa Imani kuwa yanaweza kupokelewa kwa haraka sana.

### 4.4.1 Matambiko Yanayofanywa Kwenye Miti Mikubwa

Katika miti mikubwa kama vile, mibuyu, mikuyu na muembe kulibainika kuwa na matambiko ya aina tofauti. Kwa mfano, katika muembe mkubwa mara nyingi hufanyika tambiko la kutoa jawabu kutokana na utabiri wa majanga yaliyotabiriwa pwani. Tambiko hili hufanyika usiku. Utafiti ulibaini kuwepo kwa tiba zinazofanyika hapo hapo na zipo tiba zinazotangazwa kwa jamii na kuitaka kila kaya kufanya tiba hiyo. Aidha, matambiko yanayofanyika chini ya mbuyu huhsisha maombi ya baraka katika mazao au tiba ya maradhi. Maradhi ni janga ambalo linawasumbua jamii nyingi na hata Taifa. Wanakijiji cha Makunduchi wakati yanapotokea maradhi hasa ya ukoo hukutana chini ya mbuyu mkubwa wakati wa usiku kwa lengo la kushtakia maradhi yanayowakabili. Nao wanakijiji hukutana wakati huo na kuzunguka mbuyu na kuimba nyimbo ifuatayo:

Kohokoho<br>
Bwana mkubwa njashitaki kohokoho<br>
Mie sitaki kohokoho<br>
Yuno kakohoa kuno kajamba pyupyupyu

Nyimbo hii hutumika kwa lengo la kuondosha maradhi kulingana na na imani zao baada ya kushtakia kwa mizimu wana imani kubwa ya kuondolewa shida yao hii ya maradhi na hufanikiwa.

Kihistoria ya ulimwengu kuna kipindi maradhi huwa mengi mfano homa hasa wakati majira yanapogeuka kutaka kuingia katika kipndi chengine mfano kutoka kipindi cha kiangazi na kuingia katika kipindi cha masika au kuoka kipindi cha masika na kuingia katika kipindi cha kipupwe kutokana na mgeuko huu maradhi huonekana kuingia katika jamii. Wakati inapotokea shida kama hii ambapo maradhi huenea kwa kasi ndipo wanakijiji cha Makunduchi ndipo wanapoamua kwenda katika muembe maalumu ambao hutumika kuomba kutatuliwa shida zao nyingi yakiwemo maradhi. Hivyo wanakijiji hukutana chini ya muembe huo na kuimba nyimbo hii:

Wimbo wa Mbatatao
Mbatatao maungo yaje
kuno kukonda njonini mbatatao maungo yaje
Uno mbatatao homa gani maungo yaje
Uno mbatato shetani gani maungo yaje

Hapa wanamaanisha kwamba haya mashetani ndio chanzo cha maradhi haya hivyo wanawaomba wawachie na wawaondolee maradhi haya kwani yanawasumbua watoto, vijana na hata wazee. Hivyo, wanahitaji amani na kuishi bila ya maradhi.

### 4.4.2 Tambiko Linalofanyika kwa Kuzunguka Mji

Jamii ya watu wa makunduchi na Bwejuu imeaathiriwa na imani ya dini ya kiislamu. Hivyo, masuala yao ya tambiko huchanganya na Masuala ya Dini. Kwa mfano, kusafisha mji ni suala la kitamaduni katika jamii nyingi na katika kijiji cha Makunduchi nao hutumia tamaduni hii katika muda maalumu kila unapofika. Wanakijiji cha Makunduchi kila unapofika katika sherehe maalumu za Mwaka Kongwa huwa wanatamaduni hii ya kusafisha mji. Unapofikia muda wanatembelea

katika vitongoji vyote vya kijiji cha Makunduchui huku wakisoma utajo maalumu wenye utajo wa imani ya dini ya Kiislamuhuu ufuatao :

Adhkar

Allahu aakbaru allahu Akbar

Lailaha Ila llah allahu akbar

Allahu Akbar walilahi l-hamdu

Huu ni utajo ambao humaanisha Mungu mkubwa na ndie mtatuzi wa kila jambo, hivyo Mungu ndie mwenye uwezo wa kuondosha mabalaa yote yaliyopo katika kijiji cha Makunduchi ambayo yaliyoingia katika kipndi cha kila mwaka. Hivyo hichi ni kipindi ambacho wanakijiji huomba dua zao kwa kuondosha shida zilizopokatika kijiji cha Makunduchi. Hizi ni dua ambazo hufanyika kila mwaka.

### 4.4.3 Matambiko Yanayofanyika katika Makaburi

Utafiti umeshuhudia matambiko yanayofanyika katika maeneo ya makaburi. Sehemu ya makaburini hufanywa matambiko kwa lengo la kuomba, kutaka msamaha au kujitukuza kwa mungu. Imani hii inatokana kuwa wafu wanaweza kuunganisha nafsi za walio hai kwa kuwapatia Baraka au neema. Mara nyingi makaburi haya huwa ya watu mashuhuri katika jamii au masheikh na wanazuoni wa dini (masharifu). Katika sehemu hii huibwa nyimbo (kasida) za kuwatukuza wafu pamoja na kuwasifu. Utafiti umebaini kuwa ibada hii hufanyika wakati wa laasiri, huchinywa mbuzi au kuku, kupikwa chakula na mchuzi wake huwa maziwa. Dua zinazosomwa huwa kwa mtindo wa kuimba mara nyingi duwa hizi huwa hazifahamiki maana yake kwa mtu ambaye si mwana tambiko. Mbah (1993) anaeleza kwamba, kwa Wafrika kaburini ni sehemu tukufu mno, ambapo binaadamu hapaswi huyadharau, unatakiwa kuyatunza

na kuyaheshimu. Waafrika wanaamini kuwa roho za wafu huwa zinatembea katika dunia yao na huwa zinaweza kuwasaidia wale walio hai. Kwa mujibu wa utafiti huu tumebaini kuwa Waafrika wanatukuza mno maeneo ya kaburini na ndio maana wakawa wanafanya ibada katika maeneo hayo.

Kwa mujibu wa nadharia ya simiontiki katika msimbo wa kiutamaduni kuwa fasihi ya jamii lazima iendane sambamba na tamaduni za jamii husika. Hivyo, ni wazi kuwa kuyatunza makaburi ni miongoni mwa amali za kiutamaduni zinazofanywa na wanajamii

### 4.4.4 Matambiko Yanayofanyika Mapangoni

Kabla kufanyika kwa Mwaka kogwa Wazee wa mji hutayarisha shughuli hiyo kwa kunda kwenye mapango kwa ajili ya kuratibu, kupanga na kushaurizana siku ya kufanyika kwa Mwaka kogwa. Aidha, katika sehemu hiyo ya mapango Wazee huomba ulinzi wa shughuli yao na kutaka Baraka ya tukio hilo. Pia, taarifa rasmi kwa mahoka na mizimu huwa imepelekwa kwa lengo la kuitii ahadi mambazo Wazee waliwekeana Mwaka uliopita**.** Jambo hilo linaonesha wazi kuwa jamii za watu wa makunduchi na bwejuu huamini kuwepo kwa nguvu zinazotokana na matambiko yao

Ayittey, George (2014) anaeleza kuwa, mapango katika miji ya Waafrika huaminiwa kuwa kunawza kuwa na jadi za wazee. Katika jamii ya Ghana mapango hutumiwa kama sehemu ya ibada kwa kurejelea maombi sehemu hzo hutukuzwa na kuonekana ni muhimu sana. Kwa mujibu wa maelezo hayo mapango yanaonekana ni sehemu zenye jadi pamoja na kufanyika kwa matambiko. Kupitia nadharia ya simiontiki juu

ya msimbo wa kiutamaduni kuwa jamii ni lazima iendane na utamaduni wake. Aidha katika nadharia ya uhalisiajabu ni wazi kuwa ibada zinazofanyika sehemu za mapango ni za Uhalisi lakini zinaonekana kutawaliwa na ajabu.

## 4.5 Dhima Zinazojitokeza katika Nyimbo za Matambiko ya Jamii ya Watu wa Mkoa wa Kusini Unguja

Katika sehemu hii mtafiti amefanya uchambuzi wa dhima zinazojitokeza katika nyimbo za matambiko kutoka Makunduchi ili kuonesha dhima zinavyoendana na hali halisi ya maisha katika jamii.

Kwa mujibu wa watafitiwa, nyimbo za matambiko zimekusanya dhima mbalimbali kulingana na aina ya nyimbo na haja ya maombi ya jamii husika kulingana na shida na matakwa yao kama vile kutoa wosia, kudhibiti maradhi, kuhimiza suala la mapenzi, kusafisha mji, kuondoa mabalaa mbalimbali, kuonesha uwezo wa suala la kiimani. Pia, kuonesha utabiri wa jamii yao nini kifanyike ili jamii iepukane na shida na mabalaa yanayowazunguka kijijini hapo.

### 4.5.1 Matambiko Huwafanya Wanajamii Kuwa na Utii

Dhima hii hujengwa wakati wa matambiko yenyewe. Kwa kuamini kuwa ahadi zilizofanyika kwenye tambiko ni lazima zitekelezwe. Utafiti umebaini kuwa watambikaji huwa na hofu na kukumbuka ahadi walizowekeana baina ya mahoka, mashetani na wanakijiji ahadi ambazo kila Mwaka ni lazima zitekelezwe. Pia, heshima na utiifu hufanyika pale inapotokea shida ya maradhi au dhiki wanajamii hukimbialia kwenye eneo la tambiko kwa kuomba. Dua ambazo hupokelewa kwa haraka na kupata matokeo yanayoridhisha. Hivyo, ni wazi kwamba mahoka, mizimu

na wanajamii huwa wanaheshimiana katika utekelezaji wa ahadi wanazowekeana. Ekweariri (2020) Waafrika wamejiegemeza katika falsafa ya utii kwa mkubwa, Mungu n ahata kiongozi wa jamii. Ikiwa kuna mjumuiko wa Waafrika dunia kokote wataheshimiana kwa mujibu wa umri, jinsia au elimu. Hivyo, ni wazi kuwa tambiko la Kiafrika huwa linalenga katika heshima za Wafrika kwa sababu kwenye ibada hiyo nidhamu ndio msingi wa utekeleaji wa shughuli zote za tambiko.

### 4.5.2 Kujenga Heshima za Koo

Kwa vile matambiko huwa wanakabidhiwa koo maalumu, utafiti umebaini kuwa tambiko za watu wa Kusini Unguja huongozwa na Wazee katika koo maalumu wanaoheshimiwa katika jamii. Pia, utaratibu wa tambiko hupewa heshima na kutukuzwa. Pia, nyimbo zinazoimbwa katika shughuli hiyo huwa ni za kuhimiza umoja na heshima kwa wale wanaohusisika na mizimu. Kwa mfano, familia fulani huwa ndio wenye mizimu ya sehemu fulani, watu hao huheshimiwa mno wakati wa kutekelezjai wa ibada hiyo. Jamii huwa inawaheshimu, kuwapa njeo na kuwatukuza. Adatara, Peter, Johanita na wenzake (2019) wanasema, jamii yenye kupewa dhamana ya kushuhulikia mizimu na maeneo ya ibada za jadi huwa wanapewa heshima na kutukuzwa katika jamii Ghana, wao hutumika kuombea watu wengine pamoja na kutatua matatizo ya jamii. Katika wa utafiti huu tumebaini kuwa koo zinazoshughulikia Mwaka kogwa, mizimu na maaeneo ya ibada za jadi ni koo zenye hadhi na heshima kubwa kwa jamii ya watu wa Kusini Unguja.

### 4.5.3 Ushirikiano Katika Kazi

Utafiti umebaini kuwa nyimbo za tambiko huwa zinahamasisha umoja na mashirikiano ya jamii, hasa kazi ya kumtoa shetani inapokuwa ngumu. Hivyo, fundi huhitaji kupatiwa msaada na mganga mweziwe na ndio huimba mwimbo huu.

*Wimbo mzigo mwa ntwisha*

*Hee × 2,*

*Mzigo wenu mwanitwisha, Mwanivunja mgongo,*

*Nenda ukaseme, mzigo seuweza.*

Wimbo huu umeelezewa kuwa huwa unaimbwa ikiwa fundi ameshaona kuwa kazi yake ya kumtoa shetani au kumfukuza kuwa imeshakuwa ngumu kwa sababu ya ukubwa wa shetani anayekabiliana naye na ugumu wa tiba anayotaka kuifanya kutokana na namna ambavyo maradhi ya mgonjwa yalivyo. Fundi ameshagundua kuwa pamewekwa tego, kukosea kuitegua tego hiyo inaweza kusababisha kupoteza uhai wa mtu mmoja wapo kama si mgonjwa basi fundi. Katika mazingira hayo, ili tiba ifanikiwe kunahitajika kuuondosha tego ili kuweza kumfungua mgonjwa, ambapo sio kazi rahisi kabisa. Hapo ndipo fundi hupiga ukelele na kuimba wimbo wa *Wanivunja Mgongo*. Mara zote unapoimbwa wimbo huu waganga weledi husogea kwa haraka na kumaidia fundi/ mganga kumkomoa shetani.

Kwa hivyo, fundi mkuu anawajuulisha waganga wenzake kuwa kazi imekuwa ngumu kwa kutumia wimbo huu wa kimafumbo kwa lengo la kuamuru uganga usiendelee kwa mgonjwa huyo kwani ni hatari. Ekweariri (2020) anaeleza kuwa, wanawake wa Afrika huwa wamashrikiana katika mila na desturi zote hasa ushirikiano wao huwa katika matambiko. Wanawake wanashirikiana katika uzazi,

ulezi n ahata makunzi ya jamii. Waafrika wanashirikiana katika utekelezaji wa amali zao, nyimbo zo huwa zinahamasisha umoja na ushirikiano pia.

### 4.5.4 Nyimbo Hutumika Kwa Lengo la Tiba

Licha ya kwamba jamii kubwa ya wanafasihi wanaelewa kuwa dhima ya fasihi ni kuelimisha, kuburudisha, kurithisha utamaduni na nyingezo. Lakini katika utafiti huu baada ya mahojiano ya kina na watafitiwa, amebaini kuwa nyimbo ni sehemu ya tiba. Tiba hii imejigawa katika makundi mawili. Mosi, nyimbo zenyewe hutumika kuwatibu wagonjwa wakati wa maradhi. Katika jamii za wamakunduchi na bwejuu tumebaini kuwa zipo tiba kadhaa zifanywazo kwa kutumia nyimbo. Mgojwa huimbiwa na kupigiwa viwale. Pia, nyimbo hutumika kufafanua dawa na maelekezo ya matibabu kwa baadhi ya maradhi. Kwa mfano wimbo ufuatao huimbwa katika tambiko huku mgojwa akiwa anaaguliwa dawa zake na kwa hivyo husema:

*Mzambarau dawa × 2,*

*Wende ukachimbe majununi,*

*Mzambarau dawa.*

Katika uganga au matambiko mgonjwa huwekwa kati akielekezwa kaskazi huku akiwa amefunikwa kaniki jeusi gubigubi baadaye huimbiwa nyimbo za mafumbo zinazoambatana na upigaji wa makofi au ngoma baada ya muda mfupi shetani hupanda kichwani na kusema shida yake na fundi kumuahidi kutekelezewa na hatimaye mgojwa kupoa. Kwa hivyo, mafumbo na tamathali katika nyimbo za *puuo* huwa na maana ya kama tambo ya kuficha tiba inavyoendelea kufanyika kwa mgonjwa. Kwa mfano, wimbo wa *Yana Wenyewe*. Katika wimbo huu fundi huimba ili kutoa taarifa kwa jamii ya mgonjwa kuwa kuna jambo la jadi wamelipuuza ndio

sababuya kudhurika, lakini wenye mgonjwa wakikubali kulitekeleza, mgonjwa hupata nafuu au kupona kabisa.

Kwa maelezo ya fundi aliyebahatika kusailiwa na mtafiti, alieleza kuwa uganga ni kazi, na kila mwenye kazi huwa anatumia mitindo maalum ili kuonesha kipaji chake, kwa hivyo, kila kitu kukitaja na kukisema wazi wazi itasababisha watu kuchukua utaalamu na hatimaye fundi kukosa wateja. Vile vile, aliongeza kusema kuwa, mafundi aghalabu hutumia lugha ya mafumbo sio katika nyimbo tu bali pia, katika kutoa maelekezo ya kimatibabu. Kwa mfano, majina ya mimea na miti iliyozoeleka kwa wanajamii kwa majina ya kawaida, mafundi hutumia majina mengine kwa miti au mimea hiyo, kama vile, mbuyu huitwa *mkuu hapingwa*, mvinje bahari huitwa *kiti cha jini* na mdaka komba huitwa *mnanuzi*. Canda (1988) anaeleza kuwa, matambiko ya kijamii hutumiwa na Waafrika kama tiba ya maradhi yanayowasumbua, maradhi ya kisaikolojia au maradhi ya mwili. Tiba hizi hupatikana kwa kumuimbia mgojwa na imni za jadi za watu hao humfanya mgonjwa kupata faraja katika hali yake ya kiafya.

### 4.5.5 Kuendeleza Utamaduni wa Jamii

Jilala (2016) anasema utamaduni ni uzoefu wa kimaisha wa watu wa jamii ambao jamii moja hutofautiana na jamii nyingine kuhusu masuala ya kimaisha. Hivyo, tunaweza kusema kuwa utamaduni ni mkusanyiko wa mambo yote ambayo hueleweka na kuyatumia jamii katika kuendesha shughuli zao za kila siku. Hivyo kupitia nyimbo za matambiko ya kijiji cha Makunduchi, tambiko linadhima ya kuhifadhi utamaduni wa jamii ili kurithisha kizazi hadi kizazi, nyimbo hizo hutumika kueleza mambo mbalimbali ya utamaduni pamoja na amali jalia. Kwa ujumla

tambiko lenyewe ni shughuli ya kiutamaduni, ambalo huwa kunafanyika mambo mbalimbali ya kiutamaduni ikiwemo kuimba nyimbo za kiutamaduni. Hivyo, kufanyika kwa matambiko katika jamii huwa kunawaelekeza vijana kuendeleza mila na desturi za jamii. Kwa mfano, kufanyika kwa Mwaka kogwa kumekuwa mashuhuri mno kutokana na jamii kukubaliana kwa shughuli hiyo. Hivyo, vizazi vya Kusini vinaendelea kurithi na kujitukuza dhidi ya utamaduni wao wa matambiko ya Mwaka kogwa. Katika tukio la Mwaka kogwa kufanyika mambo ambayo si ya kawaida, kama vile binaadamu kuingia katika kibanda na halafu kuchomwa moto, kupigana kwa kutumia gomba. Matendo haya kwa vijana wa makunduchi wameyachukua na kuyakubali ingawa kwa jamii nyingine yanaoneka kuwa sio ya kawaida.

Kwa mujibu wa nadharia hii ya uhalisia mazingazombwe tunaona kuwa Matukio ya kuduwaza na kuogofya au kutisha ndio yanayoweza kueleza dhima ya fasihi, matukio mbalilmbali ambayo si kawaida ambayo hutokea kama vile kuzuka kwa upepo mkali, majitu yasiyokawaida hubeba dhima ya kutambulisha utamaduni wa jamii

### 4.5.6 Kujenga Tabia ya Uvumilivu

Kama kawaida ya mwanafasihi anapowasilisha kazi yake huwa na ujumbe maalum ambao anakusudia kuufikisha katika jamii inayomzunguuka.utafiti umebaini kuwa katika jamii za bwejuu na makunduchi, nyimbo za tambiko huimbwa kwa lengo la kuhamasisha jamii kuwa na tabia ya uvumilivu, kuombana radhi na kusameheana kwa pale wanapotokea kutofahamiana.

*Wimbo usambe na cheka*

*Usambe na cheka wee,*

*Kumbe naumia wee, hoya,*

*Kumbe naumia.*

**Chanzo: uwandani: 2022**

Huu ni wimbo ambao huimbiwa shetani wa R*ubamba*. Kwa maelezo ya mzee mmoja ambaye mshabiki wa ngoma na nyimbo za *Puuo*, alisema, nyimbo za tambiko na uganga zinajenga dhima mbalimbali kwa jamii kwa sababu hutumika kurithisha amali na utamaduni wa jamii. Wimbo huu unaonesha namna mwimbaji anaonesha hisia zake huku akiitanabaisha jamii kuwa anaumia wakati akiwa amepandisha shetani. Ademowo, Johnson (2015) tambiko hutumika kutatua matatizo, kupatanisha watu na kujenga uvumilivu miongoni mwa wana jamii. Utamaduni huu umekuwepo Afrika kabla ya kuja kwa wakoloni. Wafrika walikuwa na taasisi imara za kusimamia ustawi wa maisha yao, tamaduni ambazo zimetumika kuwaunganisha pamoja.

Mwimbaji huu ameonakana naranda huku na huku akiwa na shetani kichwani. Jamii ya watu wakusini wanaamini kuwa mtua anaweza kupandisha shetani kichwa na akazungumza kwa niamba ya shetani huyo. Kwa mantiki hiyo nadharia ya uhalisajabu inajithibitishwa kwa kuamini kuwa shrtani anakaa katika mwili wa mwanadamu.

### 4.5.7 Dhima za Mapenzi na Ndoa

Sehemu hii pia tumebaini kuwepo kwa dhamira za mapenzi ndani ya nyimbo za tambiko. Nyimbo hizo huwa zinaomboleza na kuwaombea wana ndoa kuwa na neema na heri za maishani. Mfano wa wimbo wenye dhima hiyo ni

Wimbo wa wakuu

Wakyuu wa wakuyuu,

Leo tuja wakadizi,

Wanenu, wafungu ndoa,

Tunaomba muwape barka za babu zao, za Wazee wao,

Na sadaka yao upokele kwa mikono miwili,

Na ndoa yao iwe zuri waishi milele na milele.

(Chanzo: Simai 2020)

Wimbo huu ni ushahidi kuwa katika matambiko suala la ndoa na mapenzi huwa linazungumzwa katika matambiko ya watu wa jamii ya Kusini Unguja. Hivyo basi mapenzi na matambiko ni mambo yasiyotenganishwa**.** BAKIZA (2010) linaeleza kuwa mapenzi ni hisia nzito ya moyoni inayomfanya mtu avutiwe, athamini na ajali mtu kitu au jambo. Dhamira ya mapenzi ni miongoni mwa dhima maarufu zinazopatikana katika kazi ya fasihi kama vile riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi pamoja na kazi nyenginezo (Omari, 2014).

Dhamira hii imekuwa ikiwasilishwa kwa namna mbalimbali kulingana na madhumuni ya kila mwandishi anapoandika kazi yake ya fasihi. Njogu na chimerah (1999) wanasema mapenzi katika jamii hutazamwa kwa mtu na mpenzi wake kama mume na mke, mtu na wazazi wake, mtu najamii yake na mtu na taifa lake.

Kwa mujibu wa nyimbo hizi za matambiko zimeonesha mapenzi kwa upeo wa hali ya juu kwa kuonyesha mapenzi kwa kuusia wanawao kufanya yale yanayotakiwa kufanyiana kwa mume na mke ili kuzidisha mapenzi. Mfano katika nyimbo iliotajwa

hapo juu katika nyimbo hio tunaona kuwa mapenzi ni mafungamano ya pande mbili hivyo mume na mke wanahitaji kuwa wamoja na si kubughuziana hapo ndipo mapenzi yataponoga, hivyo, katika nyimbo hii tunaona kuwa wazazi wanamuusia mkwe wao kukaa na mwanawao vizuri asipigwe kwani huo si utaratibu wa ndoa na endapo atafanya hivyo iko siku mtoto huyo wa kike atasema kwa wazazi wake na ni tatizo kwani huwa ni chanzo cha kuvunjika kwa ndoa. Nyimbo hii huimbwa wakati Bi harusi na Bwana harusi wakishafunga ndoa hivyo watani wakiwa pamoja na baba na mama huambatana pamoja kwa lengo la kuwaasa wanandoa hasa mwanamme kwani yeye huonekana ndie anayebeba dhima kubwa katika familia. Hivyo nyimbo hizi za matambiko zina kazi ya kutengeneza na kurekebisha myenendo mizuri katika ndoa.

Kwa kuhusisha vipengele hivi na mihimili ya nadharia teule ya Simiotiki na uhalisia mazingaombwe. Tukianza na msimbo wa Kiseme katika nadharia hii ya simiotiki: Neno *seme* hutumiwa kukielezea kipengele nasibishi cha kisemantiki. Hivi ni vipengele ambavyo vinatuwezesha kupata picha fulani. Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji au mtazamaji atakavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani wa kifasihi. Katika kipengele hiki kinachonasibisha na msimbo huu tunaona kwamba jamii inajenga dhana fulani ya kuwa nyimbo hizi za matambiko ni chachu ya kuwajengea wanandoa mustakabali mzuri wa maisha yao katika safari mpya ya kindoa, na hujengeka kuwa bila ya wanandoa kufanyiwa matambiko ni suala ambalo ndoa hiyo haina baraka ya kutosha na huweza kupata misukosuko.

### 4.5.8 Kutoa Wasia kwa Wanadoa

Nyimbo za matambiko bado zina dhima kubwa katika jamii ikiwemo kutoa wasia mfano katika kijiji cha Makunduchi pale watu wanapotaka kufunga ndoa nyimbo hizi hutumika ikiwa kama ni njia mojawapo ya kuwaandaa wanandoa waweze kukabiliana katika maisha haya mapya ya ndoa. Taasisi ya ndoa huwa haiachwi bure ni lazima tambiko lifanyike ili kuzifanya ndoa hizi kuwa imara na kuzikabidhi sehemu yenye usalama kwa Baraka na neema. Kwa mfano wimbo huu huimbwa katika tambiko la ndoa

Mwimbo wa makame
Makame kifundefunde,
Mwana mfunde wako,
Usifunde ya mwenzako,
Ukifunda ya mwezako kauko nao mlimo.

Ingawa wimbo huu haulengi kuwafundisha wana ndoa kwa jicho la kawaida. Lakini katika jicho la uhakiki wimbo huu unatoa wasia kwa wanakijiji wa Makunduchi kwa kuwataka wanandoa kuishi vizuri na kupendana wimbo huu huimbwa mwezi mmoja kabla ndoa kufungwa watu hukutana chini ya mbuyu Wazee wa kike maalumu ambao hujishughulisha na kazi hizi huku wakifuatana na wanawake wengine watu wazima kwa lengo la kuitikia na kuzidisha mori katika nyimbo hii.kwa lengo la kuwaimbia nyimbo hizo ili kuwa makini katika maisha mapya na kuondoa misukosuko katika ndoa hiyo. Msokile (1992) ameeleza kuwa nyimbo huimbwa kwa mafumbo na huimbwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa jamii. Kinachoimbwa lazima kitoke miongoni mwa jamii. Ndani ya jamii kuna mambo mengi

yanayotendeka. Nyimbo za jando na unyago zinaimbwa na jamii ili kuhimiza mwenendo bora unaojenga maisha yenye kuleta maendeleo. Mara zote nyimbo hizo hukemea na kufunza wanawari.

Katika Msimbo wa Kiishara, Msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji au watazamaji wanagundua maana za kiishara katika kazi ya kifasihi. Katika msimbo huu watazamaji hupata nafasi ya kujenga dhana juu ya vichwa vyao baada ya kuangalia tukio fulani. Mfano katika nyimbo hizi za matambiko baadhi ya wakati huambatana na maigizo kama vile mke anavyomhudumia mume pindi tu anaporejea nyumbani. Igizo kama hili linampa mtazamaji ishara na hisia fulani na kujua kumbe namna gani jamii inatakiwa iwe baada ya kuangalia igizo tu.

### 4.5.9 Dhima ya Usafi

Wakati wa usafishaji wa mji kwa kuuulinda na maradhi yanayoweza kujitokeza wanakijiji wa makunduchi na bwejuu hufanya tambiko la kuzunguka mji. Katika tambiko hilo huimbwa kasida au kutaja maneno yaliyomo katika dini ya kiislamu. Tukio hili huwajenga vijana kujua umauhimu wa kuhifadhi na kutunza mji.

Allahu aakbaru allahu Akbar
Lailaha ila llah allahu akbar
Allahu Akbar walilahi l-hamdu

Adhkar kwa imani ya Kiislamuni kumzukuru Mungu kwa maana ya kumtaja kila wakati, katika kijiji cha makunduchi hutumia utajo huu katika kuzunguka kijiji kizima kwa lengo la kukiombea dua kijiji hicho ili kuondokana na balaa za mshetani

yanayoweza kuwadhuru na balaa nyengine kama njaa, nuksi na kuondoa mikosi. Utajo huu huendelea kutajwa kila wanapopita na mwiso wanapoishia huchinjwa mbuzi na kupikwa na kuliwa na hapo ndipo mwisho wa kusafisha mji kwa siku hiyo.

Katika mhimili mwingine wa nadharia hii ni kwamba inakiuka sifa za uhalisia, katika mhimili katika masimulizi hujitokeza mambo ambayo ni kinyume na uhalisia ambayo kwa binadamu wa kawaida humpa dhana ambayo ni vigumu kuamini**.**

Katika muhimili huu unawiyana moja kwa moja na kipengele hichi kwa kuona kitu fulani ni kweli baada yake hutokea kitu hicho kama kilivyotabiriwa au kisitokee kabisa, lakini kwa imani zao kitu hicho hutokea kweli ingawa ni vigumu mwanzo kuamini iwapo utaambiwa, mfano kutokea kweli kwa maradhi maradhi baada ya kuona dalili fulani zilizojitokeza. Temples (1969) Matambiko ya watu wa Makunduchi hufanywa kutokana na sababu mbalimbali ambazo zipo nje ya uwezo wao, sababu hizo ni kama kupatwa na maradhi wasioweza kuyatibu, kukithiri kwa maovu kijijini mwao, kuombeana dua za mafanikio kujikinga na balaa pamoja na kuwashukuru wahenga na mizimu yao.

### 4.5.10 Kuondoa Shida

Katika mila na desturi za Kifrika mwanaadamu hajikamilishi kwa shida zake hadi azieleze na kukabidhi kwa Mungu au miuungu. Dhana hiyo imewafanywa Wafrika waamini kwamba kuna nguvu za utekelezaji zaidi ya nguvu walizonazo wao. Utafiti umebaini kuwa watu wa makunduchi na bwejuu hutumia kizimu, mapango au shetani kuwakadithi shida zao kwa Imani ya kiutamaduni. Siku ya waka Kongwa watu wa Kusini hueleza shida zao na kuomba kwenye makaburi, Pwani au kwenye

miti mikubwa. Wimbo mashuhuri wanaoimbiwa wajane wakati wa kuowaombea wapate waume ni

Kifimbo chao wajane

Kifmbo chao wajane na wanapao

Wano waume na wanawao wakae kwao

Kifimbo cha wajane na watoto wadhibitiwe

Katika nyimbo wanawake wasio na waume hukutana wakati wa usiku. Katika nyimbo hii pia watoto hawatakiwa kushiriki. Hii ni nyimbo yenye dhima ya kuwakusanya wajane kwa lengo la kuomba baadhi ya shida zao mfano kuomba waume wema watakaoweza kuwaondolea shida zao, kuomba kwa ajili ya kupata riziki na kuondoa ya mizuka yanayotokana na mashetani.

Kwa kutumia nadharia hii ya simiotiki katika Msimbo huu wa Kirejelezi Msimbo huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni vinavyorejelewa katika kazi inayohusika. Urejelezi huu huunda Uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu vinavyoeleweka na wasomaji au watazamaji, hivyo kuipa kazi ya kifasihi nguzo za kiutamaduni. Msomaji/ mtazamaji anaposema anaelewa akisemacho mtunzi huwa anasema hivi kutokana na viashiria vya msimbo huu.

Katika msimbo huu tunaona kuwa nyimbo ndio imebeba msingi mzima wa dhima ambayo wanawake wasio na wanaume wanatarajiwa kuwafikia maudhui hayo. Hivyo iwapo wajane hao watairejelea nyimbo basi watapata mafunzo tosha katika kujirekebisha kulingana na mazingira na maisha wanayoishi. Hivyo nyimbo hizo huimbwa zikiwa zimebeba mafunzo tosha kwa ajili ya maisha ya wanawake hao.

## 4.6 Hitimisho

Sura hii imechambua data zilizokusanywa. Uchambuzi wa data hizi umezingatia malengo ya utafiti huu. Na umeongozwa na mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe na Simiotiki nadharia hizi zimesaidia sana katika kuchambua data za utafiti huu wenye lengo la kuchambua dhima ya nyimbo za matambiko katika kijiji cha Makunduchi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha majumuisho ya jumla ya mada ya utafiti huu unaohusu dhima ya nyimbo katika matambiko ya jamii ya watu wa mkoa Kusini unguja, vipengele vilivyoangaziwa katika utafiti huu ni pamoja na muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo na hitimisho.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu umechunguza dhima ya nyimbo za matambiko mifano kutoka katika kijiji cha Makunduchi. Utafiti ulilenga kubainisha nyimbo za matambiko ambazo huimbwa wakati wa matambiko katika kijiji cha Makunduchi nyimbo kumi zilishughulikiwa, pamoja na ubainishaji wa nyimbo hizo, zilichunguzwa na kuchambuliwa dhima mbalimbali zilizojitokeza katika nyimbo hizo za matambiko katika kijiji hicho.

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ni sura ilisheheni utangulizi wa jumla wa utafiti huu. Mambo yaliyoanishwa hapo ni pamoja na usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, pamoja na maswali ya utafti huu yanayomuongoza katika utafiti huu, vipengele vyengine katia sura hii ni pamoja na umuhimu wa utafiti. Sura ya pili imeonesha mapitio mbalimbali ya kazi tangulizi ambazo mtafiti amezipitia, kazi hizi ni zile ambazo zinahusiana moja kwa moja na mada ya utafiti. Utafiti huu umetumia nadharia ya uhalisia mazingaombwe katika uchambuzi wa data.

Sura ya tatu inaeleza mbinu za utafiti na imekusanya vipengele kama vile muundo wa utafiti, kundilengwa, sampuli na usampulishaji, njia zilizotumika kukusanya na kuchambua data zilizokusanywa kutoka uwandani ambazo zilijibu maswali ya utafiti ili kufikia malengo ya utafiti huu pamoja na maadili ya utafiti. Sura ya nne iliwasilishwa na kuchambua data zilizokusanywa toka uwandani na maktabani ambazo zilijibu maswali ya utafiti ambayo inatoa hitimisho la utafiti mzima pamoja na mchango wa utafiti. Mwisho suraya tano inatoa maoni na mapendekezo kuhusu tafiti zinazoweza kufanywa ili kuuendeleza utafiti huu.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti kwa kila lengo

Utafiti huu ulikuwa a malengo mahususi matatu ambayo ni

### 5.3.1 Lengo la Kwanza

Lengo hili liliongozwa na swali la kwanza lisemalo Ni nyimbo zipi zinazoimbwa katika matambiko ya jamii ya watu wa Mkoa Kusini Unguja. Mtafiti amegundua kuwa kuna nyimbo nyingi za matambiko katika kijiji hichi cha Makunduchi ambazo huimbwa zikiwa na malengo tofauti kwa lengo la kukiendeleza kijiji hicho na hata Taifa katika suala la utamaduni. Baadhi ya malengo yake nyimbo hizi ni kutatua shida nyingi zinazokikabili kijiji hicho ikiwemo njaa, maradhi na shida nyenginezo.

### 5.3.2 Lengo la Pili

Lengo hili liliongozwa na swali linalosema, ni wapi, wakati gani nyimbo za matambiko ya jamii ya watu mkoa wa Kusini Unguja huimbwa? Katika kujibu suali hili mtafiti amegundua kuwa kuna wakati na sehemu maalumu kama vile kwenye miti mikubwa kama vile miembe, mibuyu, kwenye mapano, baharini na hata wakati

mwengine kuzunguuka mji hasa katika tukio ambalo hufanyika mara moja kwa Mwaka tukio la kusafisha mji kwa lengo la kuondoa mabalaa yanayokikumba kijiji hicho.Vilevile, mtafiti amegundua kuwa wakati maalumu ambazo nyimbo hizo huimbwa kama vile maadhimisho ya Mwaka kogwa na wakati zinapotokeashida mbalimbali kama  maradhi, njaa, jua kali, miti kutoanyika vizuri watu hukutana kwa lengo la kwenda katika miungu kwa ajili ya kuomba ili kuondoshewa shida hizo.

### 5.3.3 Lengo la Tatu

Lengo hili la tatu na la mwisho katika utafiti huu liliongozwa na swali hili, Ni dhima zipi zilizopo katika nyimbo za matambiko ya watu wa Mkoa Kusini Unguja. Katika lengo hili mtafiti amegundua kuwa nyimbo za matambiko zina dhima nyingi miongoni mwao ni kutoa wosia, kuondosha maradhi, kurekebisha malezi ya wanandoa, suala la mapenzi, pamoja na kuhifadhi na kurithisha utamaduni. Hali zote hizi zimesaidia katika kukieka kijiji hichi kuwa katika hali ya usalama na kuwa na maendeleo hadi sasa.

## 5.4 Matokeo ya Jumla

Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa nyimbo za matambiko bado zinaendelezwa katika kijiji cha Makunduchi licha ya vijana wa leo kuonekana kupinga ambao ndio watagemewa wa kushika na kuendeleza shamere hii. Nyimbo hizi tumeona kuwa huimbwa sehemu na wakati maalumu kama chini ya miti mikubwa na mapango lakini huimbwa wakati yanapotokea majanga yanayoikumba jamii kama maradhi, njaa na jua kali. Na pia nyimbo hizo zina dhima ya kutoa elimu kwa ajili ya wanandoa, kutoa wosia, kuepusha maradhi na kuhifadhi na kuendeleza

silika na desturi za watu wa kijiji cha Makunduchi ambalo ni jambo jema kwa kijiji hicho na Taifa kwa ujumla.

## 5.5 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umetoa mchango katika sekta tofautitofauti kama ifuatavyo:

Elimu: utafiti utawaweshesha wana taaluma kupata rejea inayohusu nyimbo, tambiko na fasihi simulizi kwa ujumla. Aidha katika taaluma wanafunzi wanaweza kuona umuhimu wa kuhifadhi amali za matambiko kwa jamii.

Watunga sera: utafiti utasaidia kuona umuhimu wa kuzihifadhi amali ambazo zinaonekana kupotea katika jami. Aidha, mikakati ya kuihifadhi inaweza kusaidia kukua na kuenea kwa taaluma ya fasihi jalia.

Kutokana na utafiti uliofanywa umegundua mambo mengi na unapendekeza mambo yafuatayo:

Kuendelezwa kkwa mila na desturi za matambiko katika sehemu nyingi za Tanzania kwani mila hizi zinaonekana zinaleta faida nyingi kama vile kuondoa maradhi na shida zinazoikabili jamii kutokana na imani zao.

Serikali kuingilia kati baadhi ya matambiko kwani yanaonekana yanaitangaza nchi hasa kuhusu suala la utamaduni wa Taifa kwa mfano Makunduchi kwa vile yanaonekana matambiko haya yameambatana na tukio muhimu la kihistoria la kiutamaduni la Mwaka kogwa.

Serikali ianzishe kamati za kiutamaduni za shehia, kata, tarafa na hata Wilaya kwani inaonekana mila hizi zinaanza kupotea, hivyo kamati hizi zitasaidia kuwahamasisha vijana kuendeleza mila hizi kwani zinapotea kwa kasi kubwa hapa Tanzania.

## 5.6 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Kwa hakika matokeo ya utafiti huu yametoa mwanya na njia kwa watafiti wajao kuendelea kufanya tafiti mbalimbali kama ifuatavyo:

Watafiti wanayo nafasi ya kuchunguza sababu ya kupuuza mila za tamaduni za matambiko. Pia wanaweza kuchunguza athari hasi za matambiko kwa jamii ya watu wa Tanzania.

## 5.7 Hitimisho

Sura hii ni ukamilishaji wa utafiti mzima. Ambapo sura imeanza kwa kutoa muhtasari wa utafiti, ikifuatiwa na matokeo ya utafiti, vilevile sura imeonesha mchango wa utafiti, na kuonesha mapendekezo ya maeneo ya kufanyiwa utafiti na hatimae kumalizia kwa kutoa hitimisho.

## MAREJELEO

Adamson, P. B. (1985). “Some rituals associated with parturition in antiquity”. *Folklore 96: 176–93*

Adatara, na wezake (2019). Cultural beliefs and practices of women influencing home births in rural Northern Ghana. International Journal of Women’s Health 11: 353–61.

Ademowo, Johnson (2015). “Conflict Management in Traditional African Society”, https://www.researchgate.net/publication/281749510.

Ali, H. (1969). *Lugha Yetu*, juz 1 na 1 uk 20.

Ali, S. A. (2013). “Athari za Mtindo Katika Kuibua Maudhui: Mifano kutoka Bembelezi za Pemba.” Tasnifu ya umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Al-Maqqarī, Aḥmad Ibn-Muḥammad. 1840. *The History of the Mohammedan Dynasties in Spain Extracted from the Nafhu-t-tib min Ghosni-l-Andalusi-r-Rattib wa Tarikh Lisanu-d-Din Ibni-l-Khattib*.

Ameir, I. H. (1983). *Misingi ya Nadharia ya Uhakiki*. Dar es Salaam : TUKI.

Ayittey, G. (2014). “African Solutions, African Problems, Real Meaning”, katika https://www.panafricanvisions.com

BAKITA, (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.

BAKIZA, (2010). Kamusi ya Kiswahili Fasaha, Oxford University Press: East African Limited, Kenya.

Balisidya, M. (1987). “Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi”, Katika jarida la *Mulika namba.19*.

Bogdan, R. na Biklen, S. K. (1992). *Qualitative Research of Education: An Intropduction to Theory and Methods* (Edrs), Boston: Allyn and Bacon.

Bryman, A. (2004), *Social Research Methods* (2nd edition), Oxford: Oxford University Press.

Buliba, A. na wenzake (1996). Misingi ya nadharia na mbinu za Utafiti. Mwanza: Serengeti Educational Publishers. 86

Canda, E. R. (1988). Therapeutic Transformation in Ritual, Therapy, and Human DevelopmentJournal of Religion and Health, Vol. 27, No. 3 (Fall, 1988), pp. 205-220 (16 pages). Springer Publisher

Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu**.** Tasnifu ya Uzamivu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Cohen, L. na wenzake (2000). *Research Methods in Education 5 edition*. London: Rutledge Falmer.

Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publication.

Eberhard-Gran, na wezake (2010. Postnatal care: A cross-cultural and historical perspective. Archives of Women's Mental Health 13: 459–66

Ekweariri, D. (2020). The Passive Origin of the Institutionalization of Power Inequality in the Meaning/Experience of Womanhood in Igboland. Frontiers in Sociology 5: 1–13.

Enon, J. C. (1998). Educational Research Statistics and Measurements, Kampala: Makerere University.

Gideon, M. (2020). Tazama, ISSN 0856-9193, Toleo Nanba 921, "Freemansons na*hirizi ya miungu 36 inayotakiwa kuvaliwa shingoni"*, jumanne, julai, 21-27, 2020.

Hassan, M. (2013). Taswira zinazojitokeza katika nyimbo za Mwaka Kogwa. Tasinifu ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Isalamic Propagation Centre (IPC), (2009). *Historia yakuhuisha uislamu*, Dar es Salaam: Afroplus industries.

Juma, A. (2018). Kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo za Taarab asilia za Shakila Said. Tasinifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzani.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*, Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (2004). *Research Methodology*: Methods and Techniques, New Delhi: New age International (P) Limited Publishers.

Kothari, R. C. (2008). *Research Methodology:* Methods and Techniques, New Delh: New age International Publishing Ltd.

Kothari, R. C. (2013). *Research Methodology*: Methods and Techniques, 2 nd Ed, New Age International (P) Ltd: New Delhi.

Magdalena, O. na Chinemerem (2021). Article Rituals and Embodied Cultural Practices at the Beginning of Life: African Perspectives. Religions 12: 1024. https://doi.org/10.3390/rel12111024

Masebo J. A na Nyangwine N (2000), Nadharia ya Fasihi, The General Booksellers. Ltd. Dar es salaam, Tanzania.

Mbah, na wezake (1993). "Igbo Child Initiation, Christian, and Baptism": A Case Study in Inculturation. Extracto de la Tesis Doctoral presentada en la Facultad de Teología de la Universidad de Navarra. Ph.D. Thesis, Faculty of Theology, University of Navarra, Pamplona, Spain

Mbarouk, A. A. (1983), Nyimbo za Michezo ya Watoto: Katika Fasihi Simulizi, Zanzibar TAKILUKI, Dar es Salaam:

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI

Mutembei, K. A. (2012), Korasi katika Kiswahili: Nadharia mpya ya Uhakiki, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. “Athari za Nyimbo za Mipasho kwa Jamii ya Wazanzibar,” Taasisi ya Elimu na Ukuzaji Mitaala (1988), Kiswahili Sekondari. Zanzibar: Taasisi ya Ukuzaji Mitaala.

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Njogu, K. & Chimerah, R. R. (1999).*Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Jimo Kenyatta Foundation: Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R; (1999) Ufundishaji wa Fasihi Nadharia **na** Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyata University.

Ruhumbika, G. (2002). *Janga Sugu la Wazawa*, Dar es Salaam: E & D Limited.

Sengo T. S. Y. (1975) *Shaaban Robert: uhakiki wa maandishi yake***.** Longman, -

Sengo, T. S. Y. & Lucas S. A. (1975). *Utani na jamii Ukwere*, Dar es Salaam: Foundation Books.

Sengo, T. S. Y. M. (2008). *Tafakuri ya Utu na Uhai*, Dar salaam: Huda Publishers.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (toleo la 3)*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi istilahi na nadharia*. Nairobi : Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2007). *Kichocheo cha Fasihi*. Nairobi: English Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Zakaria, M. (2017). Kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto. Tasinifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzani.

# VIAMBATANISHO

## Kiambatishi namba moja

**Kohokoho**

Bwanamkubwa njashitaki kohokoho

mie sitaki kohokoho

yuno kakohoa kuno kajamba pyupyupyu.

**Kiswahili sanifu**

Bwanamkubwa nijashitaki kohokoho

mie sitaki kohokoho

huyu kakohoa huku kajamba pyupyupyu

**Mbatatao**

Mbatatao maungo yaje

kuno kukonda njonini mbatatao maungo yaje

uno mbatatao homa gani maungo yaje

uno mbatato shetani gani maungo yaje

**Kiswahili sanifu**

Mbatatao maungo yaje

Huku kukonda ndo nini mbatatao maungo yaje

huu mbatatao homa gani maungo yaje

huu mbatato shetani gani maungo yaje

**wosia**

Makame kifundefunde

mwana mfunde wako

usifunde wa mwenzako

ukifunda ya mwezako kauko nao mlimo

**Kiswahili sanifu**

Makame kifundefunde

mtoto mfunde wako

usifunde wa mwenzako

ukifunda ya mwezako huondoka na ujuzi wake

**Kimwana**

Mwanangu mdogo asijepigwayo magongo

naakija kwao kachajasemayo si muongo

mumeo akaja kuwa upenuni uuke

ukaamuuze kwema na usalikher umke

**Kiswahili sanifu**

Mwanangu mdogo asijekwendapigwa magongo

naakija kwao atakujasema uyo si muongo

mumeo akaja ukiwa upenuni uondoke

ukamuulize hali mumeo na usalikher umpe

**Pungwa**

Pungwa watotoe ee

mwenye mwana aushe

pungwa watoto ee

ng’ombe yule nitoe

**Kiswahili sanifu**

Pungwa watotoe ee

Mwenye mtoto aondoshe

Pungwa watoto ee

Ng’ombe yule nitoe

**Kifimbo chao wajane**

Kifmbo chao wajane na wanapao

wano waume na wanawao wakae kwao

kifimbo cha wajane na watoto wadhibitiwe

**Kiswahili sanifu**

Kifimbo chao wajane na watoto wao

Hawa waume na watoto wao wakae kwao

Kifimbo cha wajane na watoto wadhibitiwe

**Mwana kidete**

Mwaka na mwana kidete mnasemaje

laila Pwani kuja udagaa na usitende

**Kiswahili sanifu**

Mwaka na mtoto wa kidete mnasemaje

Laila Pwani umekuja udagaa na usitandwe

**Kibanda hodi hodi**

Kibanda hodihodi na wenyewe tuwamo

Tumekuja kwa vishindo na kakara

Hatulikuja kwa kuomba

Ndo desturi ya mwaka

Salama salama yamjaliwae

Azae mke na ndume na kisimani atume

Na dukani atume

na kunini atume

kevu kalala  kamlamseni

alawe nje aje usa wageni

**Kiswahili sanifu**

Kibanda hodihodi na wenyewe tumo ndani

Tumekuja kwa vishindo na kakara

Hatukuja kwa kuomba

Ndo desturi ya mwaka

Salama salama yamjaliwae

Azae mke na mume na kisimani atume

Na dukani atume

Na kunini atume

kama kalala kamuamsheni

aje nje aje ondosha wageni

**Adhkar**

Allahu aakbaru allahu Akbar

Lailaha ila llah allahu akbar

Allahu akbar walilahi l-hamdu

**Kiswahili sanifu**

Allahu aakbaru allahu akbar

Lailaha ila llah allahu akbar

Allahu Akbar walilahi l-hamdu